Kanuni za Usimamizi, Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi katika Ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

Zilizorejelewa 2022



ECF
ELECTORAL COMMISSIONS FORUM OF SADC COUNTRIES

EISA
Electoral Institute for Sustainable Democracy in Africa

Kanuni za Usimamizi, Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi katika Ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

Zilizorejelewa 2022

Imechapishwa na Taasisi ya Uchaguzi na Demokrasia
Endelevu Barani Afrika (EISA)

Abidjan, Côte d'Ivoire
Lot numéro 2974, ilot 247, aux II Plateaux-7ème Tranche.
Cocody, Abidjan, Côte d'Ivoire

Johannesburg, Afrika Kusini
14 Park Road • Richmond 2092
S.L.P. 740 • Auckland Park 2006, Afrika Kusini
Simu +27 11 381 60 00 Faksi +27 11 482 61 63
Barua Pepe info@eisa.org Tovuti www.eisa.org

EISA 2023

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kuzalishwa, kuhifadhiwa katika mfumo rejeshi au kusambazwa katika namna au kwa njia yoyote ile ya kielektroniki, kimakenika, au kunakiliwa, kurekodiwa, au vinginevyo, bila idhini ya maandishi ya mchapishaji

Imechapishwa kwa ukarimu na msaada wa kifedha wa watu wa Marekani kupitia kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID)

Usanifu na mpangilio: Tume Huru ya Uchaguzi (IEC) ya Botswana

Mzunguko wa Uchaguzi uliandaliwa na: European Commission (EC), International Institute for Democracy and Electoral Assistance (International IDEA), United Nations Development Programme (UNDP)

Yaliyomo

Dibaji....6

Shukrani....9

Vifupisho....11

1. Utangulizi....13

2. Mazingira ya Kitaasisi kwa ajili ya Uchaguzi katika Nchi za SADC....20

2.1 Mfumo wa Kikatiba na Kisheria....20

2.2 Mifumo ya Uchaguzi....21

2.3 Vyombo vya Usimamizi wa Uchaguzi....25

2.4 Teknolojia katika Chaguzi....27

2.5 Usimamiaji wa Vyama vya Siasa....29

2.6 Utatuzi wa Migogoro ya Uchaguzi....32

2.7 Wajibu wa Washirika wa Maendeleo wa Kimataifa....33

3. Kabla ya Uchaguzi....35

3.1 Elimu ya Uraia na Wapiga Kura....35

3.2 Usajili wa Wapiga Kura....37

3.3 Mgawanyo wa Majimbo....39

3.4 Ushiriki wa Vikundi Vilivyopuuzwa katika Uchaguzi....40

3.5 Ushiriki wa Asasi za Kiraia katika Uchaguzi....42

3.6 Uteuzi na Usajili wa Wagombea....43

3.7 Kampeni....44

3.8 Ushiriki wa Vyombo vya Habari katika Uchaguzi..... 46

3.9 Matumizi ya Intaneti na Mitandao ya Kijamii..... 48

3.10 Upotoshaji wa Habari na Hotuba za Chuki;..... 49

3.11 Vurugu za Kisiasa..... 51

4. Kipindi cha Uchaguzi..... 53

4.1 Hatua za Kiusalama..... 53

4.2 Nyenzo na Vifaa vya Kupigia Kura..... 54

4.3 Maeneo ya kupigia kura..... 56

4.4 Wasimamizi wa Uchaguzi..... 58

4.5 Taratibu za Upigaji Kura..... 60

4.6 Usiri wa Kura..... 62

4.7 Wakala wa Chama/Wagombea..... 64

5. Usimamizi wa Matokeo..... 66

5.1 Kuhesabu kura na Usimamizi wa Matokeo..... 66

5.2 Utangazaji wa Matokeo ya Jumla..... 67

6. Baada ya Uchaguzi..... 69

6.1 Migogoro Baada ya Uchaguzi..... 69

6.2 Marejeleo na Tathmini ya Baada ya Uchaguzi..... 70

7. Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi..... 72

7.1 Mawanda na Methodolojia/Mbinu..... 72

7.2 Uteuzi na Muundo wa Misheni za Waangalizi wa Kimataifa..... 76

7.3 Mfumo wa Utoaji Taarifa..... 78

8. Hitimisho 80

Viambatisho 81

Kiambatisho 81

Dibaji

Kanuni za Usimamizi, Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi katika Ukanda wa SADC (PEMMO), zilizopitishwa mwaka 2003 zimetumiwa sana hadi sasa na EMBs, Asasi za Kiraia na watendaji wengine katika Ukanda wa SADC. PEMMO imechangia ipasavyo katika kuaminiwa kwa uchaguzi katika Ukanda wa SADC, kwa mfano Waangalizi wa Uchaguzi wa EISA na ECF-SADC wanarejelea PEMMO kutathmini mienendo ya uchaguzi tangu 2004. Pia, PEMMO inatumika kama waraka mwongozo kwa watendaji na watafiti. Licha ya matumizi na mapendekezo yake ya kina, ikizingatiwa kuwa hatua kadhaa zimepigwa tangu 2003 ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa kanuni nyingine pamoja na PEMMO na mazingira endelevu ya kufanya chaguzi (kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiteknolojia) na muktadha mwingine, EISA na ECF-SADC zilibaini haja ya kupitia upya PEMMO ili kukidhi mazingira ya kimataifa ya uchaguzi ambayo yamebadilika kwa kiasi kikubwa. Katika miaka ya hivi karibuni, baadhi ya mwelekeo mpya katika usimamizi wa uchaguzi ni pamoja na yafuatayo;

- Mashirika zaidi ya Kusimamia Uchaguzi yanatumia teknolojia za kidijitali kuendesha uchaguzi,
- Vyama vya kisiasa vinatumia majukwaa ya mitandao ya kijamii na akili bandia ili kuwashirikisha wapiga kura kwa njia za kibinafsi na zinazowalenga zaidi,
- Vikundi vya waangalizi wa uchaguzi pia vimepanua wigo wao wa tathmini ili kujumuisha, kwa mfano, TEHAMA, ufadhili wa kampeni, ufadhili wa vyama vya

siasa na ushirikishwaji wa makundi yaliyopuuzwa katika mchakato wa uchaguzi,

- Janga la Uviko-19 limesababisha tafakari mpya juu ya uendeshaji wa uchaguzi katika muktadha wa dharura ya kiafya,
- Kwasasa, EOMs pia zinafanya uangalizi wa uchaguzi wa muda mfupi na mrefu, na
- Uchaguzi unazidi kuwa wa gharama kubwa na kuna mahitaji makubwa ya usalama kwa waendesha uchaguzi na vifaa.

Mapitio ya kina ya PEMMO yalifanywa katika kipindi cha mwaka 2019 - 2022 ili kuhakikisha kwamba waraka wa PEMMO uliorejelewa unaonesha masuala yanayoibuka katika nyanja inayokua ya usimamizi na uangalizi wa uchaguzi.

Tunayofuraha kuwasilisha waraka wa PEMMO uliorejelewa unaopatikana katika lugha nne (4) za SADC, ambao unatoa mapendekezo muhimu ya Kisera juu ya masuala kadhaa yanayojitokeza. Tuna uhakika kwamba waraka wa PEMMO uliorejelewa utatumiwa na EMBs na wadau wengine wakuu wa uchaguzi ili kuimarisha ushiriki zaidi na mijadala kuhusu kuimarisha demokrasia na usimamizi wa uchaguzi katika ukanda huu.

Tunaishukru kwa dhati timu ya kiufundi iliyofanya kazi bila kuchoka ili kukamilisha waraka huu wa PEMMO uliorejelewa. Niruhusu nitoe shukrani zetu kwa Kikosi Kazi cha PEMMO chini ya uratibu wa Sekretarieti ya EISA na ECF-SADC. Washirika wetu katika mradi huu, USAID, wanastahili kutajwa na kushukriwa kiupekee kabisa.



Dr. Elsie T. Nghikembua

Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya ECF-SADC

Mwenyekiti - Tume ya Uchaguzi ya Namibia

Baidessou Soukolgue

Mkurugenzi Mtendaji

Taasisi ya Uchaguzi na Demokrasia Endelevu Barani Afrika (EISA)

Shukrani

Mapitio ya PEMMO ni matunda ya ushirikiano kati ya ECF-SADC na EISA. Kikosi kazi cha mapitio cha PEMMO kinapenda kutoa shukrani za pekee kwa wajumbe wa Kamati Tendaji ya ECF-SADC kwa mwaka 2018-2020 chini ya uongozi wa Wakili Notemba Tjipueja, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Namibia, Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa EISA, Bw. Denis Kadima, na Mkurugenzi Mtendaji wa sasa wa EISA, Bw Baidessou Soukolgue, kwa msaada na mwongozo wao. Kikosi kazi cha kurejelea PEMMO kina deni kubwa kwa Sekretarieti ya ECF-SADC inayoongozwa na Katibu Mtendaji, Bi Hilda Modisane, na Kiongozi wa EISA katika Mradi wa STEP, Bw Justin Doua Goré, kwa kuratibu na kusimamia mradi katika ngazi ya taasisi.

ECF-SADC na EISA tunatoa shukruni zetu za dhati kwa tume zote wanachama wa ECF-SADC na asasi za kiraia zilizoshiriki katika mashauriano ya wadau na kutoa michango yao muhimu katika hatua mbalimbali za mchakato wa kurejelea. Shukrani za pekee ziende kwa Tume za Uchaguzi za Mauritius, Namibia, Zambia na Zimbabwe kwa kuruhusu makamishna na wafanyakazi wafuatao kuhudumu katika kikosi kazi cha kurejelea PEMMO:

- Kamishna Ulrich Freyer, Tume ya Uchaguzi ya Namibia
- Kamishna Joyce Laetitia Kazembe, Tume ya Uchaguzi ya Zimbabwe
- Bw Bob Musenga, Katibu wa Tume ya Uchaguzi ya Zambia

- Bi Neena Seewoo, Naibu Afisa Mkuu wa Uchaguzi, Ofisi ya Kamishna wa Uchaguzi wa Mauritius
- Bw Petrus Shaama, Mkurugenzi wa Uendeshaji, Tume ya Uchaguzi ya Namibia
- Bi Zenia Klazen, Naibu Mkurugenzi: Usajili na Mipango, Tume ya Uchaguzi ya Namibia

ECF-SADC inatoa shukrani zake za dhati kwa wajumbe wa kikosi kazi na mtaalam wa uandishi, Dk Catherine Musuva, kwa utaalam wao, bidii na kujitolea.

PEMMO hii iliyosasishwa imewezekana kwa msaada wa ukarimu kutoka kwa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID). ECF-SADC na EISA wanawajibika kwa yaliyoandikwa humu na si lazima yaakisi mtizamo wa USAID au Serikali ya Marekani.

Vifupisho

AU	Umoja wa Afrika
AZAKI	Asasi za Kiraia
BVR	Usajili wa Mpiga Kura wa Bayometriki
CBO	Shirika la Kijamii
CEO	Afisa Mtendaji Mkuu
ECF-SADC	Jukwaa la Tume za Uchaguzi la Nchi za SADC
EISA	Taasisi ya Uchaguzi na Demokrasia Endelevu Afrika
EMB	Shirika la Kusimamia Uchaguzi
EOM	Misheni ya Uangalizi wa Uchaguzi
EXCO	Kamati Tendaji
FBO	Shirika lenye Muelekeo wa Kiimani
FPTP	Wa-Kwanza-Ndiye-Mshindi
IDP	Watu Waliohamishwa ndani ya Mipaka
IT	Teknolojia ya Habari
MMP	Mgawanyo Sawia wa Kura za Mgombea na Chama
PEMMO	Kanuni za Usimamizi, Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi katika Ukanda wa SADC
PR	Uwakilishi wa Uwiano
SADC	Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

SMM Mgombea Mmoja Mwenye zaidi ya Nusu ya Kura Zilizopigwa Huchaguliwa

SMP Mgombea Mmoja Mwenye Kura Nyingi Huchaguliwa

TEHAMA Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

1. Utangulizi

Kusini mwa Afrika imepiga hatua kubwa katika kutaasisisha demokrasia katika miongo miwili iliyopita. Hii inaakisiwa katika maendeleo kadhaa yaliyofikiwa katika nchi za SADC, ikiwa ni pamoja na kufanyika kwa chaguzi za vyama vingi zilizofanikiwa. Kuna ushahidi kuwa kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi katika utawala na mijadala kati ya serikali na wadau kumekita mizizi. Taasisi za kidemokrasia zimeanzishwa na mabadiliko kadhaa makubwa ya kikatiba, kisheria na kiutawala yamefanyika kwa lengo la kuimarisha na kusimika demokrasia. Uzoefu katika ukanda huu na kwingineko umeonesha kuwa kuimarisha demokrasia inahusisha zaidi ya kufanya uchaguzi wa mara kwa mara na kuunda taasisi kadhaa. Inahusisha pia kuendeleza tunu zinazokubalika kwa ujumla ambazo zinahakikisha kufanyika chaguzi huru na unaozingatia uwakilishi, uwajibikaji, ujumuishaji, uwazi, usawa wa kijinsia, kuvumiliana na kuheshimu tofauti/anuwai.

Jukwaa la Tume za Uchaguzi la Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (ECF-SADC) na Taasisi ya Uchaguzi na Demokrasia Endelevu Barani Afrika (EISA) kwa pamoja walitengeneza Kanuni za Usimamizi, Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi (PEMMO) ambazo zilipitishwa tarehe 6 Novemba 2003 na kuanza kutumika Januari 2004. Kanuni hizo zilikuwa kilele cha miaka mitatu ya mradi wa utafiti shirikishi na mashauriano uliofanywa na ECF-SADC na EISA na wadau wengine muhimu wa uchaguzi wa kikanda. PEMMO ni mjumuiko wa viwango vya kusimamia mwenendo wa uchaguzi na kukuza mazingira wezeshi ambayo uchaguzi

unafanyika Afrika. Viwango hivi vinajumuisha vipengele muhimu vya mihula ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na mfumo wa kitaasisi, michakato inayohusiana na kipindi kabla ya uchaguzi, kipindi cha uchaguzi na baada ya uchaguzi. PEMMO pia inajumuisha miongozo juu ya ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi.

PEMMO imetumika kama mojawapo ya kanuni muhimu za kikanda katika tathimini za uchaguzi zilifanywa na Misheni ya Uangalizi wa Uchaguzi ya ECF-SADC (EOMs) kusini mwa Africa na EISA EOMs Afrika nzima. ECF-SADC na EISA EOMs hukuza uwezo wa usimamizi wa tume za uchaguzi za wanachama kwa kuboresha desturi bora za kiutendaji kikanda na kusaidia ECF-SADC EOMs kufundishana. Wanatoa ripoti na ufuatiliaji juu ya mapendekezo yao kwa EMBs baada ya uchaguzi, na hivyo kuweka msingi wa mageuzi ya mfumo wa uchaguzi na ushiriki baada ya uchaguzi wakati wa muhula wa uchaguzi ujao.

Kanuni nyingine za kikanda, bara na kimataifa zinazohusiana na uchaguzi zimetungwa tangu PEMMO. Hizi ni pamoja na Kanuni na Miongozo ya SADC inayoongoza Uchaguzi wa Kidemokrasia, iliandaliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2004 na kurejelewa mwaka 2015; Mkataba wa Afrika wa 2007 juu ya Demokrasia, Uchaguzi na Utawala; Mwongozo wa Upatikanaji wa Taarifa na Uchaguzi Barani Afrika, uliopitishwa mwaka 2017; na Azimio la 2005 la Kanuni za Uangalizi wa Uchaguzi wa Kimataifa lililoidhinishwa na mashirika ya kiserikali na mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali. Mnamo 2020, Umoja wa Afrika (AU) ulitengeneza Miongozo ya Uchaguzi wakati wa Dharura za Afya ya Umma, kwa mfano, janga la UVIKO-19. SADC pia ilitengeneza Miongozo ya Uangalizi wa Uchaguzi wakati wa

Dharura za Afya ya Umma. Mashirika ya kimataifa kama vile Taasisi ya Kimataifa ya Demokrasia na Usaidizi wa Uchaguzi (International IDEA) na Taasisi ya Kimataifa ya Mifumo ya Uchaguzi (IFES) pia walitengeneza miongozo kama hiyo. ECF-SADC na EISA EOMs hurejelea kanuni hizi katika tathmini zao za uchaguzi, pale inapofaa.

Tangu kupitishwa kwa PEMMO, mazingira ya uchaguzi yamebadilika na hili likiwa na athari kubwa kwa usimamizi na uangalizi wa uchaguzi. Chaguzi katika ukanda huu zimekuwa na ushindani zaidi na pia kumekuwa na kuongezeka kwa ushindani baina ya vyama na ndani ya vyama. Kukosa hamasa katika kushiriki uchaguzi na kujitokeza kwa idadi ndogo ya wapiga kura pia kumekuwa ni kawaida katika chaguzi za baadhi ya nchi. Imani katika Vyombo vya Usimamizi wa Uchaguzi (EMBs) imeongezeka katika baadhi ya maeneo na kupungua kwa mengine. Kukataa kukubali matokeo ya uchaguzi kumesababisha matokeo ya uchaguzi kupingwa mahakamani na baadhi ya wagombea. Kumekuwa na kesi ambapo mahakama zimebatilisha uchaguzi na tukio moja ambapo EMB yenyewe ilibatilisha matokeo ya uchaguzi. Kesi zote hizi mbili zilisababisha uchaguzi kurudiwa na hatimaye kutia dosari katika uadilifu wa EMBs. Kutokuwa tayari kwa EMB kumesababisha uhahirishwaji wa dakika za mwisho wa chaguzi au kumesababisha ucheleweshaji mkubwa wa kupiga kura katika baadhi ya nchi. Katika hali mbaya zaidi, majengo ya umma yanayotunza vifaa vya uchaguzi yameharibiwa na wakati mwingine wasimamizi wa uchaguzi wameshambuliwa, na hivyo kuibua vitisho vipya vya kiusalama kwa EMBs.

Chaguzi pia zimekuwa za kisasa zaidi katika zama hizi za kidijitali, na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imetumiwa. Matumizi ya teknolojia yameibua shauku na wasiwasi miongoni mwa wadau wa uchaguzi. Kwa mfano, ununuzi wa teknolojia na vifaa vya uchaguzi kutoka nje ya nchi kumefanya chaguzi kuwa ghali sana na zaidi kumepenyeza makampuni ya nje katika mchakato wa uchaguzi. Baadhi ya nchi pia zimekuwa zikitegemea sana fedha za wafadhili ili kuendesha uchaguzi. Ushiriki huo wa wageni unaweza kuathiri uendelevu na uwezo wa nchi kumiliki mchakato wa uchaguzi.

Kuenea kwa mitandao ya kijamii kumekuza demokrasia ya kidijitali kwa kuboresha uwezo wa wananchi kupata taarifa kwa kutoa fursa za mijadala na ushiriki katika siasa. Hata hivyo, mitandao kijamii pia imekuwa nyenzo za kueneza taarifa potofu na hotuba za chuki. Vivyo hivyo, vikundi vya waangalizi wa uchaguzi pia vimepanua wigo wao wa tathmini kwa kujumuisha teknolojia ya chaguzi, ufadhili wa kampeni na vyama vya siasa, kuhusisha makundi yaliyopuuzwa katika mchakato wa uchaguzi, mitandao ya kijamii na propaganda, kati ya mengine. Pia, wanafanya uangalizi wa muda mfupi na muda mrefu wa uchaguzi kwa kutumia mkabala wa muhula wa uchaguzi.

Mwishowe, katika kuibuka kwa janga la UVIKO-19 mnamo 2020, kulinda uadilifu wa uchaguzi katika muktadha wa dharura za afya ya umma kumekuwa muhimu. Kwa uharaka, Serikali husika katika ukanda wa SADC zilichukua hatua za kukabiliana na dharura ambazo zilikuwa na athari katika kuendesha chaguzi za kidemokrasia zinazoaminika. Vyombo vya

Usimamizi wa Uchaguzi (EMBs) katika ukanda huu pia viliweka mikakati na hatua za kupunguza athari za janga la UVIKO-19 juu ya uendeshaji wa chaguzi katika nchi husika. Aidha, AU, SADC na mashirika ya kimataifa yaliandaa miongozo ya kufanya uchaguzi na uangalizi wa uchaguzi chini ya dharura za afya ya umma.

Ni katika muktadha huu unaobadilika ambapo ECF-SADC na EISA walitambua haja ya kurejelea na kusasisha PEMMO kuakisi mienendo ya sasa katika nyanja inayokua ya usimamizi na uangalizi wa uchaguzi. Kuhusiana na dharura za afya zinazojitokeza, ECF-SADC na EISA waliamua kutumia miongozo iliyopo ya kitaifa, kikanda na kimataifa badala ya kutunga miongozo ya ziada katika PEMMO kwa ajili ya tathmini za uchaguzi.

Kikosi kazi cha pamoja cha ECF-SADC na EISA kilianzishwa mnamo Machi 2019 ili kutengeneza mfumo wa kurejelea, kushauriana vya kutosha na wadau wa kikanda wa uchaguzi na kuandaa Kanuni zilizofanyiwa mapitio (angalia Kiambatisho A). Kikosi Kazi kilikamilisha mchakato wa utungaji katika mkutano uliofanyika Gaborone, Botswana mnamo 25-26 Mei 2022. Rasimu ya mwisho iliwasilishwa katika mikutano ya Kamati ya Maafisa Wakuu wa Uchaguzi na Kamati Tendaji ya ECF-SADC mnamo Julai 2022 ili kuthibitishwa. PEMMO iliyorejelewa ilithibitishwa na EXCO na hatimaye kupitishwa mnamo Oktoba 2022 katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa ECF-SADC huko Namibia.

Kumbuka kwamba PEMMO imeandaliwa kwa kuzingatia kwamba kila nchi ina mazingira ya kipekee ya kisiasa, kisheria, kijamii na kitamaduni. Hivyo basi, inatarajiwa kwamba nchi zitatumia nyaraka hii kwa mujibu wa hali za nchi husika kwani imeandaliwa katika namna ambayo inaakisi mpangilio wa matukio katika usimamizi wa chaguzi. Inaanza kwa kujadili mahitaji muhimu ya kisiasa na kikatiba ambayo yataunda mfumo wa uchaguzi na taasisi husika. Kisha inaangalia hatua tatu za mchakato wa uchaguzi – kabla ya uchaguzi (maandalizi), kipindi cha uchaguzi (kupiga kura) na baada ya uchaguzi (uhakiki na tathmini). Hatua zote hizi tatu ni za msingi kwenye taratibu na michakato muhimu ili kufanikisha uchaguzi huru na haki, unaoaminika na halali katika mazingira yenye utulivu na amani. Mwelekeo na changamoto mahsusi za kikanda zinatambuliwa katika hatua zote tatu na mapendekezo yanayojielekeza kwenye desturi bora za kiutendaji katika usimamizi wa chaguzi. Kwa kuwa zinagusa hatua zote, kipengele cha ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi kimefafanuliwa tofauti na kujumuishwa katika waraka huu kabla ya Hitimisho.

Kanuni zinazopendekezwa hushughulikia masuala makuu yafuatayo:

- hitaji la mfumo wa kisheria wa kina na mazingira wezeshi;
- ujumuishwaji na ushiriki wa makundi yote ya jamii, ikiwa ni pamoja na makundi yaliyopuuzwa;
- umuhimu wa uwazi na upatikanaji wa taratibu za awali za maandalizi ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na

mchakato wa mgawanyo wa majimbo, usajili wa mpiga kura, uteuzi wa wagombea na elimu ya mpiga kura;

- utoaji taarifa wa vyombo vya habari vya zamani na jukumu la vyombo vipya vya habari katika uchaguzi;
- vyanzo vya fedha kwa ajili ya vyama vya siasa na kampeni;
- propaganda (upotoshaji) na hotuba za chuki;
- kipindi cha maandalizi na usimamizi wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na mahala na ufikikaji wa vituo vya kupigia kura, mpangilio wake, kupiga kura na usiri wa kura, na kufunga, kuhesabu, na mchakato wa kuyapanga;
- kipindi baada ya uchaguzi, ikiwa ni pamoja na utatuzi wa migogoro ya uchaguzi na tathmini ya mchakato wa uchaguzi; na
- mchakato wote wa uchaguzi, hasa ufuatiliaji na uangalizi, usiwe na mawaa (vizuizi) wala upendelo, uaminike na uzingatie weledi.

2. Mazingira ya Kitaasisi kwa ajili ya Uchaguzi katika Nchi za SADC

2.1 Mfumo wa Kikatiba na Kisheria

Katiba na sheria ni nyaraka za msingi za nchi ambazo hutoa mawanda na mazingira ya kisheria ambamo uchaguzi hufanyika. Katiba ya nchi yoyote inapaswa kutoa mfumo wa kisheria kwa nchi hiyo na kutumika kama msingi wa kufanyika uchaguzi ambao ni huru, wa haki, wa kuaminika na halali.

Nchi nyingi za SADC zimekubali kusimamia haki za msingi na uhuru binafsi ambazo zinapatikana kwenye katiba zao pamoja na kufanya chaguzi za vyama vingi ambazo ni huru, za haki, za kuaminika, shirikishi, jumuishi na halali. Nchi nyingi zina sheria zinazowezesha kusimamia mwenendo mzima wa uchaguzi katika jitihada za kufikia matakwa ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Kanuni Zinazopendekezwa

Mfumo wa kikatiba na kisheria unapaswa:

- kuhakikisha uhuru wa msingi na haki za binadamu, kukuza utawala bora na tunu za utulivu wa kisiasa;
- kutoa njia za kushughulikia migogoro/malumbano ya uchaguzi;
- kutoa fursa kwa ajili ya mapitio ya katiba kwa kuzingatia kanuni za utendaji wa kidemokrasia;
- kuruhusu usawa wa kijinsia kwa uwazi na kuchukua hatua maalum kulinda makundi yaliyopuuzwa kama

suluhisho la muda mfupi, hadi uwakilishi wa uwiano utakapopatikana;

- kuwa na kifungu cha wazi juu ya aina ya mfumo wa uchaguzi;
- kuwa na kalenda ya udumu ya uchaguzi, kubainisha tarehe ya uchaguzi au kipindi cha kufanya chaguzi;
- kutokukiuka kanuni za msingi za haki na uhuru wa binadamu, kwa mfano, masharti maalum kwa ajili ya kuheshimu haki za binadamu kama vile uhuru wa kukusanyika na kujieleza, ambao utahusisha haki ya kuunda na kujiunga na chama fulani cha siasa au kuwa wagombea binafsi;
- kuandikwa kwa lugha rahisi na kutafsiriwa katika lugha ya taifa;
- kuruhusu uanzishwaji wa chombo huru na kisicho na upendeleo cha usimamizi wa uchaguzi; na
- kutunga vifungu vya kikatiba na kisheria ambavyo hushughulika hasa na kwa undani na masuala ya uchaguzi na vinapaswa kutambua haki ya kukata rufaa kwa watu ambao hawajaridhika.

2.2 Mifumo ya Uchaguzi

Mfumo wa uchaguzi ni njia ambayo kura hutafsiriwa katika viti vya bunge. Kwa hiyo, chaguo la mfumo huamua asili ya uwakilishi na muundo ambao kwao viti hutengwa. Kuna mifumo mikuu minne ya uchaguzi inayotumika duniani kote.

(a)Mgombea Mmoja Mwenye Kura Nyingi Huchaguliwa (SMP)

Kwa kawaida hujulikana kama 'Wa-Kwanza-Ndiye-Mshindi ' (FPTP), mfumo huu unachukuliwa kuwa rahisi zaidi. Nchi

inagawanywa katika majimbo ya uchaguzi, ambayo kila moja huchagua mgombea mmoja tu kama mwakilishi wake katika bunge. Mshindi katika kila jimbo la uchaguzi ni mgombea ambaye anapata angalau kura moja zaidi kuliko wagombea wengine wote na sio lazima kupata kura zaidi kuliko wengine wote pamoja. Mfumo huu unaweza kumaanisha kwamba chama kilicho na idadi ndogo ya kura nchi nzima kinakuwa chama tawala. Ingawa hauvinufaishi vyama vidogo, mfumo wa SMP unasifiwa kwa kujikita katika dhana ya uwajibikaji kwa mwakilishi wa jimbo aliyechaguliwa.

(b) Mgombea Mmoja Mwenye zaidi ya Nusu ya Kura Zilizopigwa Huchaguliwa (SMM)

Katika mfumo wa Mgombea Mmoja Mwenye zaidi ya Nusu ya Kura Huchaguliwa (SMM) nchi imegawanywa katika majimbo. Faida ya SMM dhidi ya mfumo wa SMP ni kwamba mshindi lazima apate kura nyingi kabisa katika jimbo. Ingawa mfumo huu hautumiki kwa kawaida katika ukanda wa SADC, baadhi ya majimbo huutumia kwa uchaguzi wa urais. Pale ambapo mgombea wa urais anashindwa kupata wingi wa kutosha, uchaguzi wa duru ya pili unahitajika.

(c) Mfumo wa Uwakilishi wa Uwiano (PR)

Ingawa kuna aina mbalimbali za mifumo ya PR, aina inayotumiwa sana ni mfumo wa orodha ya chama uliofungwa. Katika mifumo mingi ya PR nchi nzima inachukuliwa kuwa ni jimbo moja kwa hivyo hakuna haja ya kufanya mchakato wa kutenga majimbo kama ilivyo katika mifumo ya FPTP na SMM. Kwa ujumla, mfumo wa PR unahakikisha kuwa vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi vina uwakilishi bungeni, kwa

uwiano wa idadi ya kura zote halali zilizopigwa. Ingawa mfumo huu husifiwa kwa kuhakikisha uwakilishi bora na kuhakisi vyema mtizamo wa umma, huleta ukaribu kati ya Wabunge na vyama vyao badala ya wapiga kura.

(d)Mgawanyo Sawia wa Kura za Mgombea na Chama (MMP)

Mfumo wa MMP unachanganya mambo muhimu ya mifumo ya FPTP na PR. Mfumo huu unaruhusu baadhi ya wabunge kuchaguliwa kupitia mfumo wa FPTP huku wengine wakichukua viti vya wabunge kupitia mfumo wa orodha ya vyama uliofungwa. Ingawa wapiga kura wengi wa kawaida wanaona MMP inachanganya, hujikita kwenye mambo mazuri ya PR na FPTP, yaani uwakilishi mpana na uwajibikaji. Kwa upande mwingine, MMP pia inajumuisha mambo mabaya ya PR na FPTP.

Mifumo miwili ya uchaguzi inayotumika zaidi katika ukanda wa SADC ni mfumo wa SMP au FPTP na mfumo wa PR. Aina ya mfumo unaotumika una athari katika ushiriki, haswa ule wa wanawake na makundi mengine yaliyosahaulika. Ushahidi katika SADC unaonesha kuwa nchi zinazotumia mfumo wa PR zina wanawake wengi bungeni na katika serikali za mitaa kuliko zile zinazotumia FPTP.

Wakati mifumo hii ya uchaguzi imetawala katika uwakilishi wa bunge, baadhi ya serikali za SADC pia hutumia mfumo wa viti maalum, ambao inaruhusu chama tawala kuteua idadi maalum ya wabunge kuchukua viti maalum katika bunge. Katika hali hii, vyama tawala katika ukanda wa SADC vimekuwa vikipata faida ya kisiasa visiyostahili ikilinganishwa na vyama vya upinzani, ambayo imesababisha kutoridhika, mvutano na

migogoro ya kisiasa katika baadhi ya nchi. Hata hivyo, katika nchi chache, mfumo huu umetumika vyema kuwaweka wanawake na wawakilishi wa makundi mengine yaliyosahaulika katika bunge na serikali za mitaa.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Kila nchi ya SADC inapaswa kupitisha mfumo wa uchaguzi kulingana na kipindi husika, mpangilio wake wa kisiasa, historia, na mfumo wa kichama.
- Mfumo wa uchaguzi unapaswa kuingizwa katika Katiba.
- Sheria ya Uchaguzi inapaswa kuweka wazi aina, maudhui na uendeshaji wa mfumo wa uchaguzi uliopitishwa.
- Wadau wote, hasa wapiga kura, wanapaswa kuelewa aina ya mfumo wa uchaguzi unaotumika; jinsi serikali inavyoamua ugawaji wa viti vya bunge; aina ya uwakilishi na athari za kisiasa za mfumo uliochaguliwa.
- Mifumo ya uchaguzi inapaswa kukuza na kulinda haki za msingi za binadamu pamoja na usiri wa kura.
- Hatua maalum kama vile upendeleo chanya na kutenga nafasi za wanawake na makundi mengine yaliyosahaulika zinapaswa kuchukuliwa kama sehemu ya mifumo ya ndani ya chama na uchaguzi wa kitaifa, na kuweka mikakati ya utekelezaji wake.
- Kanuni zifuatazo lazima ziwe msingi wa mfumo wa uchaguzi:
  - uwakilishi mpana wa masilahi mbalimbali ya kisiasa na makundi tofauti ya watu;
  - ujumuishwaji na ushiriki kisiasa wa wahusika muhimu;

- uwajibikaji wa kisiasa wa wawakilishi waliochaguliwa kwa wapiga kura;
- mchakato wa uchaguzi na matokeo ulio wazi na halali; na
- kuingizwa kwa utamaduni wa demokrasia ya ndani ya chama ambayo inahakikisha uaminifu na uhalali wa mchakato wa uteuzi ndani ya vyama vya siasa.

2.3 Vyombo vya Usimamizi wa Uchaguzi

Nchi za SADC zimeanzisha vyombo vya usimamizi wa uchaguzi (EMBs) katika sheria ili kusimamia na kuendesha uchaguzi. Wengi wao wanatumia modeli ya tume huru za uchaguzi (IEC). Baadhi ya vikwazo vikuu kwa uendeshaji wao ni pamoja na uhuru mdogo, mamlaka yasiyo wazi na rasilimali na uwezo duni. Utata umeibuka kuhusiana na taratibu za uteuzi na muda wa wajumbe wa EMB kushika nafasi zao, ambayo wakati mwingine inadhoofisha uhalali, kuaminika, na uadilifu wa mchakato wa uchaguzi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMB inapaswa kutumia mamlaka yake kwa uhuru na uadilifu, na kufanya kazi zake bila hofu, upendeleo au ubaguzi.
- Taratibu za uteuzi na kufukuzwa kazi zinapaswa kuelezwa wazi na mchakato unaofanywa kwa kuzingatia uadilifu, uwajibikaji na uwazi. Taratibu hizi zinapaswa pia kuzingatia haja ya kuhakikisha mwendelezo kwa kujumuisha uteuzi wa makamishna. Ikiwa makamishna wanachaguliwa na vyama vya

siasa, wanapaswa kuwakilisha wigo mzima wa kisiasa. Mifumo kinga inapaswa kuwekwa ili kuhakikisha uhuru wa EMB hauathiriwi, na makamishna hawavurugwi na itikadi za kisiasa.

- Kuzingatia kuteua watu huru wanaojulikana ndani ya jamii kwa uadilifu wao. Inashauriwa kwamba angalau mmoja wa makamishna awe mtu ambaye anatumikia au amewahi kutumikia mahakama ya juu (jaji wa mahakama kuu au jaji wa mahakama ya upeo). Angalau asilimia fulani ya makamishna wa EMB wanapaswa kuwa wajumbe wa wakudumu ili kuhakikisha kudumu kitaasisi na kimuundo.
- Bajeti ya EMB inapaswa kupitishwa na Bunge kwa wakati.
- Serikali inapaswa kufadhili vya kutosha EMB ili iweze kufanikisha uchaguzi wa kuaminika na halali. Ufadhili wa EMB unapaswa kufanywa kwa wakati na kulingana na muhula wa uchaguzi. EMB inapaswa kuzingatia uendelevu wa kifedha na kusimamia chaguzi kwa gharama nafuu. Ukubwa wa EMB unapaswa kuwa wa wastani ili kuhakikisha usimamizi wa uchaguzi wenye ufanisi, uwezo, makubaliano, na endelevu kifedha.
- EMB inapaswa kuwajibika kwa Bunge kupitia kamati maalum ya bunge badala ya wizara na inapaswa kuripoti kila mwaka juu ya shughuli zake.
- EMB inapaswa kukuza usawa wa kijinsia na ujumuishwaji wa kijamii katika taasisi na kuhakikisha

kuwa sekta zote za jamii zinaweza kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi.

- EMB inapaswa kuwa na mfumo wa kitaasisi wa kusimamia viashiria vya hatari katika maeneo yake yote ya kazi. EMB inapaswa kuwa na mfumo wa kutambua hatari za ndani na nje na kuchukua hatua za kuzizuia na kuzipunguza.
- Usalama wa EMB unapaswa kuwekwa na kuhakikishwa wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.
- EMBs zinapaswa kufikika na ziweze kutoa kwa wadau wote sheria na kanuni za uchaguzi.
- EMBs zinapaswa kuhimizwa kuchangia rasilimali na ujuzi kwa EMBs nyingine, ikiwa inawezekana.

2.4 Teknolojia katika Chaguzi

EMBs nyingi za ukanda wa SADC hutumia TEHAMA mbalimbali kuboresha uendeshaji wa chaguzi, ikiwa ni pamoja na mifumo ya kanzidata, ramani za setilaiti, zana tumizi za simu (programu), Usajili wa Mpiga Kura wa Bayometriki (BVR), vifaa vya utambuzi wa mpiga kura na hata kupiga kura kielektroniki. Kiwango cha matumizi ya Intaneti na simujanja katika ukanda huu kiko juu, hii inafanya matumizi ya majukwaa ya mitandao ya kijamii kama vile Facebook, WhatsApp na Twitter kuenea. EMBs hutumia majukwaa na tovuti hizi kwa ajili ya kumfikia mpiga kura na kutoa taarifa za mpiga kura. Vyama vya siasa hutumia mitandao ya kijamii kwenye mchakato wa uchaguzi na kusambaza taarifa kwa hadhira kubwa ya mtandaoni kwa muda mfupi. AZAKI hutumia majukwaa haya kuhamasisha

ushiriki na kufanya uchaguzi wa amani, wakati wapiga kura wanashiriki katika mijadala na mazungumzo ya kisiasa kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii.

Ingawa teknolojia hizi zinaweza kuleta mabadiliko na ufanisi, pia kuna hatari zinazoweza kutokea. Wasiwasi umeibuliwa kuhusu gharama, uwazi, urahisi wa utumiaji, na usalama wa mtandao, kati ya masuala mengine. Mitandao ya kijamii imekuwa upanga wenye makali kuwili ambao unaweza kutumika kuboresha au kudhoofisha sana michakato ya uchaguzi. Wapiga kura wanaweza kudanganywa au kupotoshwa na wanasiasa na wagombea katika zama hizi za upotoshaji, udanganyifu na kusambaza habari mbaya kidijitali.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMBs lazima zizingatie kwa uangalifu hatari zinazotokana na matumizi ya teknolojia zinazopatikana kwao na kuja na hatua za kupunguza athari za teknolojia wanayochagua kutumia.
- EMBs zinapaswa kuchukua teknolojia ambazo ni endelevu na za gharama nafuu.
- EMBs zinapaswa kuanza matumizi ya teknolojia kwa wakati na yanatanguliwa na mchakato thabiti wa majaribio ili kuruhusu EMBs kushughulikia ipasavyo na vya kutosha matatizo au makosa yoyote yanayohusiana na teknolojia.
- EMBs zinapaswa kuruhusu tathimini ya teknolojia na taratibu za ununuzi kuchunguzwa ili kuongeza uwazi na

kukubaliwa na vyama vya siasa, wagombea na asasi za kiraia.

- EMBs lazima ziwahusishe wadau wote juu ya teknolojia yoyote inayotumiwa na wapiga kura na kuhakikisha kuwa ni rahisi kutumia.
- EMBs lazima zianzishe njia bora za ulinzi wa data.
- EMBs lazima zichukue hatua za kulinda mifumo yao ya TEHAMA na data dhidi ya uhalifu wa kimtandao.

2.5 Usimamiaji wa Vyama vya Siasa

Demokrasia ya vyama vingi yenye afya inahitaji wingi wa vyama vya siasa. Katika nchi nyingi wanachama wa SADC, vyama vya siasa vinatakiwa kujiandikisha ili kushiriki katika uchaguzi. Mchakato wa usajili huwa katika sheria na kwa kawaida huweka muda wa ukomo wa usajili. Muda ambao vyama vya siasa vinapewa kujiandikisha unaweza kupingwa ikiwa vyama havipewi wasaa wa kutosha wa kukidhi mahitaji yote. Aidha, ikiwa gharama za usajili zinaonekana kuwa kubwa sana, vyama vidogo vinaweza kushindwa kujiandikisha. Mchakato wa usajili wa vyama haupaswi kukiuka kanuni ya uhuru wa kujumuika.

Serikali kadhaa wanachama wa SADC hufadhili vyama vya siasa kulingana na uwakilishi wao bungeni. Hii ni muhimu ili kuweka mazingira sawia na kuimarisha mchakato wa kidemokrasia, lakini mfumo huu unaelekea kupendelea vyama vikubwa. Ufadhili wa serikali (umma) mara nyingi hautoshi na vyama vya siasa hupaswa kukusanya fedha kutoka kwa michango na vyanzo vingine. Vyama vya siasa vina usiri

kuhusu vyanzo vya fedha binafsi na huzuia jitihada za kutunga sheria kusimamia uwazi katika kutoa taarifa za vyanzo vya fedha. Watu na mashirika tajiri wanajulikana kufadhili vyama vya siasa na wagombea. Ushawishi unaoongezeka wa fedha katika siasa unaharibu mchakato wa kisiasa na unawapa nguvu watu wachache na udhamini wa kisiasa. Wakati mwingine, ufadhili vyama vya siasa umesababisha mivutano, hasa kati ya vyama tawala na vya upinzani, na kati ya vyama vinavyoshirikiana. Pia imeibua tuhuma za mapato ya rushwa yanayoelekezwa kwenye mchakato wa uchaguzi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Chombo huru na kisicho na upendeleo kinapaswa kuwa na jukumu la usajili na usimamiaji wa vyama vya siasa kwa kufuata mfumo wa udhibiti.
- Vigezo vya kusajiliwa na sababu za kufuta usajili kwa vyama vya siasa vinapaswa kutolewa katika sheria pamoja na utaratibu wa malalamiko.
- Wakati ofisi inayohusika na usajili wa vyama vya siasa inapaswa kuzingatia mahitaji fulani ya udhibiti kama vile mgombea au chama kuwa na amana, sahihi za wapiga kura waliojiandikisha, na uwasilishaji wa majina ya chama na nembo, kanuni hizi hazipaswi kuwa ngumu sana na kuengua vyama kushiriki katika uchaguzi.
- Vigezo vya usajili wa vyama vya siasa vinapaswa kufafanuliwa wazi na kutumika kwa uwazi na vinapaswa kujumuisha mifumo ya rufaa.
- Vyama vya siasa vinatakiwa kusaini kanuni za maadili ya uchaguzi baada ya kusajiliwa.

- Mfumo wa udhibiti unapaswa kutoa utaratibu wa kushughulikia migogoro ya ndani ya chama na baina ya vyama.
- Ufadhili wa vyama vya siasa na/au wagombea utaainishwa katika mfumo wa sheria.

- Utoaji wa fedha za umma kwa vyama vya siasa ufanyike kwa wakati muafaka.
- Chombo huru na kisicho na upendeleo kinapaswa kuwa na jukumu la kusimamia matumizi ya fedha hizi za umma na wanufaika wa fedha hizo watoe akaunti zinazoweza kuthibitishwa na chombo huru na kisicho na upendeleo.
- Kipaumbele kitolewe kwa uanzishwaji wa sheria zinazosimamia utoaji wa taarifa za vyanzo vyote vya fedha za vyama vya siasa.
- Mfumo wa sheria unapaswa kupunguza matumizi ya pesa katika kampeni ili kuzuia rushwa na ushawishi mbaya wa kifedha.
- Mfumo wa sheria unapaswa kujumuisha motisha kwa wanaotii na adhabu kwa wasiotii.
- Fedha za kampeni zinapaswa kuwa sawa, lakini fedha baada ya uchaguzi zinapaswa kuwa sawa na ushindi ambao chama kimepata kwenye uchaguzi, kwa kawaida kiasi husika kiendane na kura au viti kilichovuna.
- Kanuni za vyama vya siasa zinapaswa kuhakikisha kuwa miundo ya vyama inazingatia ujumuishaji wa kijamii na kijinsia.

2.6 Utatuzi wa Migogoro ya Uchaguzi

Migogoro inayohusiana na uchaguzi ni moja ya tishio kubwa kwa demokrasia na utulivu wa kisiasa. Kihistoria, EMB na taasisi za uamuzi kama vile mahakama, na hasa mahakama za uchaguzi, zimeshughulikia migogoro na malumbano yanayohusiana na uchaguzi..

Mbinu mbadala za usimamizi na utatuzi migogoro kama vile usuluhishi, uamuzi na upatanisho zinaweza kufikika, zenye gharama nafuu na uharaka zaidi katika kushughulikia migogoro husika. Ni nchi chache tu ambazo zinatumia mbinu hizi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Mfumo wa sheria unapaswa kutambua mifumo ya kimahakama na isiyo ya kimahakama ili kutoa haki kwenye hatua tofauti katika muhula wa uchaguzi.
- EMB, vyama vya siasa, wagombea na asasi za kiraia zinapaswa kuwezesha uanzishwaji wa utaratibu wa kuzuia na usimamiaji wa migogoro ili kukabiliana na migogoro inayohusiana na uchaguzi, ikiwa ni pamoja na mikakati kama vile kamati za uratibu za wadau na mabaraza ya migogoro.
- Wapatanishi na wasuluhishi huru, wenye ujuzi na waliofunzwa vizuri wanapaswa kufanya kazi katika kamati za usimamiaji wa migogoro zilizoanzishwa na EMB.
- Makubaliano yaliyofikiwa kupitia upatanishi, usuluhishi na uamuzi yanapaswa kuwa na nguvu ya kisheria.
- Taratibu za rufaa zinapaswa kuanzishwa kwa chaguzi zote na zinapaswa kushughulikiwa na mahakama kwa wakati.
- Mfumo wa sheria unapaswa kutaja muda kwa wazi na unaofaa wa kutatua kesi za uchaguzi au migogoro.

2.7 Wajibu wa Washirika wa Maendeleo wa Kimataifa

Mashirika ya kimataifa na washirika binafsi wa maendeleo husaidia nchi za SADC kuendesha uchaguzi kama sehemu ya misaada ya maendeleo ya kimataifa. Msaada huu unaweza kuchukua sura ya rasilimali za kifedha, nyenzo, vifaa na utaalamu. Inaweza kulenga EMBs, taasisi za kiserikali, vyama vya siasa na vikundi vya kiraia. Ingawa msaada wa uchaguzi unalenga kuimarisha taasisi na kuboresha ubora wa uchaguzi,

si mara zote umma hufahamishwa mipango ama malengo husika. Wakati mwingine wamekosolewa kwa uratibu hafifu; kuchukulia uchaguzi kama tukio badala ya mchakato; na kubeba gharama kubwa na masharti ya wafadhili.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Washirika wa maendeleo wa kimataifa wanapaswa kuheshimu dola na kuzingatia sheria za nchi husika.
- Washirika wa maendeleo wa kimataifa wanapaswa kuwa wazi juu ya mchango wao wa hali na mali (kifedha) kwenye uchaguzi wa nchi husika.

3. Kabla ya Uchaguzi

3.1 Elimu ya Uraia na Wapiga Kura

EMBs zote za SADC hutoa elimu ya kiraia na wapiga kura kwa msaada wa asasi za kiraia na mashirika ya kidini, vyama vya siasa na vyombo vya habari. Upatikanaji wa habari huwezesha watu kushiriki katika shughuli za kisiasa na kuchagiza matokeo ya uchaguzi na utawala wa nchi kwa kupiga kura. Mipango mingi ya elimu ya uraia na wapiga kura haijitoshelezi katika maudhui na idadi ya marudio, na kwa hivyo huwa na utegemezi zaidi kwa ufadhili wa nje. Wapiga kura wanahitaji kuhamasishwa juu ya teknolojia yoyote ambayo EMB itatumia kusajili wapiga kura na kupiga kura. Wapiga kura wa vijijini, hasa wale wanaoishi katika maeneo yasiyofikika, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu mara nyingi hawapati elimu ya mpiga kura. Ujinga (kutokujua kusoma na kuandika) pia ni kikwazo katika utoaji wa elimu ya mpiga kura. Inakubalika kwamba matatizo haya yanachangia wapiga kura kutokujali chaguzi, tatizo ambalo ni sugu zaidi miongoni mwa vijana wa ukanda huu.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Elimu endelevu ya uraia na mpiga kura inapaswa kupewa kipaumbele cha juu ili kupanua demokrasia, kuimarisha ushiriki na kufanya chaguo sahihi.
- EMB inapaswa kubaki na wajibu wa jumla wa kuratibu elimu ya kiraia na wapiga kura ili kuhakikisha uthabiti na udhibiti wa ubora.

- EMB, kwa kushauriana na wizara husika ya serikali, inapaswa kuandaa mtaala mpana wa elimu ya uraia na demokrasia kwa ajili ya kutumika mashuleni.
- Serikali zinapaswa kutoa kipaumbele katika ufadhili wa elimu ya uraia na wapiga kura kwa kuiweka katika bajeti ya EMB kabla ya uchaguzi.
- Elimu ya uraia na wapiga kura inapaswa kutolewa kwa njia iliyoratibiwa na thabiti, huru na isiyozingatia itikadi ya chama chochote.
- Jitihada zinapaswa kufanywa kuhakikisha kuwa wapiga kura wa vijijini wanapewa kipaumbele maalum na kwamba ushiriki wa wanawake na vijana katika uchaguzi unahimizwa.
- Kutokujua kusoma na kuandika, hasa katika maeneo ya vijijini, kunapaswa kufidiwa na matumizi ya lugha za kikabila, katuni, video, nk.
- Taasisi za kiraia kama vile Asasi za Kiraia (AZAKI), Mashirika ya Kijamii (CBOs) na Mashirika ya Imani (FBOs) pamoja na viongozi wa jadi, wa kidini, na jamii wanapaswa kuidhinishwa na EMB kusaidia utoaji elimu ya uraia na wapiga kura ili kuhakikisha elimu husika inatolewa kwa usawa na ufanisi nchi nzima.
- Vikundi vya kiraia na vyama vya siasa vilivyoidhinishwa vinapaswa kutoa elimu ya uraia na wapiga kura kwenye majimbo yao ambayo inaendana na elimu na taarifa kwa wapiga kura inayotolewa na EMB.
- Taarifa ya uraia na wapiga kura inapaswa kusambazwa zaidi kwa kadri inavyowezekana kwa kutumia vyombo vya habari vya jadi, vyombo vya habari vya kijamii na mitandao ya kijamii.

3.2 Usajili wa Wapiga Kura

Kusudi la uandikishaji wapiga kura ni kuwatambua watu ambao wanastahili kupiga kura siku ya uchaguzi. EMB ina jukumu la kuandaa kitabu cha kitaifa cha wapiga kura na kufanya uandikishaji wa wapiga kura. Katika nchi nyingi za SADC, uwazi na uhalali wa mchakato wa uandikishaji wapiga kura umepingwa, na kusababisha kutokubalika kwa matokeo ya uchaguzi. Migogoro inayohusiana na mchakato wa uandikishaji wa wapiga kura ni pamoja na vigezo vya kisheria vya kupiga kura, muda uliotengwa kwa ajili ya zoezi zima na ukaguzi wa kitabu cha wapiga kura, na usahihi wa kitabu cha wapiga kura. Nchi nyingi za SADC pia haziandikishi raia wao wanaoishi nje ya nchi kama wapiga kura, hasa kutokana na ugumu na hatari zilizopo.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Mchakato wa uandikishaji wapiga kura unapaswa kukuza ushiriki mpana na haupaswi kuzuia ushiriki wa wapiga kura wanaostahili.
- Mchakato wa uandikishaji wapiga kura unapaswa kulenga makundi yaliyopuuzwa kama vile wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na watu waliokimbia makazi yao, miongoni mwa mengine.
- Wapiga kura wanaostahili kuandikishwa wanapaswa kupewa kituo cha uandikishaji kinachofikika na endelevu.
- Lazima kuwe na muda wa kutosha kwa wapiga kura wanaostahili kujiandikisha, kwa ajili ya umma kukagua

kitabu cha wapiga kura, kuweka pingamizi na kutoa uamuzi juu ya rufaa husika.

- EMB inapaswa kusasisha na kukagua orodha ya wapiga kura kabla ya uchaguzi ujao.
- Mbinu za utambuzi wa wapiga kura zenye gharama nafuu zinapaswa kuanzishwa ili kuwezesha uandikishaji wa wapiga kura wanaostahili, huku ikipunguza uandikishaji mara mbili au haramu wa wapiga kura, kwa mfano, uwepo wa kitambulisho cha kitaifa chenye matumizi mengi sambamba na daftari la kitaifa la idadi ya watu.
- Sheria iweke utaratibu wa vyama vya siasa kufuatilia mchakato wa uandikishaji wa wapiga kura kupitia mawakala wa vyama waliowateuwa.
- Vyama vinapaswa kupewa kitabu cha wapiga kura bila malipo.
- Haki za kupiga kura zinapasa kujikita katika mambo yafautayo:
  - uraia;
  - umri wa kisheria wa mtu mzima, ambao unaweza kutofautiana kati ya nchi na nchi;
  - wakaazi wa ndani na nje ya nchi; na
  - sababu yoyote ya kupoteza sifa, kwa mfano, watu wenye rekodi ya uhalifu.

3.3 Mgawanyo wa Majimbo

Katika nchi nyingi, EMB inawajibika kwa mgawanyo wa majimbo. Hata hivyo, baadhi ya nchi huteua tume maalum kushughulikia mgawanyo huo, wakati mwingine hujulikana kama mipaka. Uanzishwaji, muundo na hadhi ya EMB inatumika ni sawa na tume ya mipaka. Mara nyingi, utaratibu wa kuanzisha tume inayohusika na mipaka zimewekwa kwenye Katiba.

Ni muhimu kutambua kwamba mchakato wa mipaka ni zoezi la kiufundi ambalo linaweza kutumika kufikia malengo ya kisiasa. Kwa hivyo ni muhimu kwamba mchakato uongozwe na vigezo vilivyo wazi. Mgawanyo wa majimbo unapaswa kuhakikisha kuwa kila jimbo lina takriban idadi sawa ya wapiga kura wanaostahili. Mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

- Idadi ya watu (msongamano wa watu);
- urahisi wa usafiri na mawasiliano;
- sifa za kijiografia;
- mpangilio uliopo wa makazi ya watu;
- utoshelevu wa kifedha na uwezo wa kiutawala wa eneo la uchaguzi;
- athari za kifedha na kiutawala za kuweka jimbo;
- mipaka iliyopo; na
- uwepo wa jumuiya yenye maslahi sawa.

Kanuni Zinazopendekezwa

Mchakato wa kutenga majimbo lazima:

- kusimamiwa na EMB au chombo huru na kisicho na upendeleo ambacho kinawakilisha jamii, na kujumuisha watu wenye ujuzi unaofaa;
- kufanyika kwa misingi ya vigezo vilivyobainishwa wazi kama vile mgawanyo wa idadi ya watu, jumuiya yenye maslahi sawa, urahisi, sifa za kijiografia na mipaka mingine ya asili au ya kiutawala;
- ufikike kwa umma kupitia mchakato wa mashauriano;
- usigubikwe na udanganyifu wa mipaka ya uchaguzi ili kupendelea makundi fulani au maslahi ya kisiasa;
- ufanywe na chombo kimoja; na
- uguse nyanja zote za kiserikali – kitaifa, kikanda, na mitaa.

3.4 Ushiriki wa Vikundi Vilivyopuuzwa katika Uchaguzi

Mchakato wa uchaguzi unachukuliwa kuwa jumuishi na shirikishi ikiwa kila raia anayestahili kushiriki katika hatua mbalimbali katika muhula wa uchaguzi anaweza kufanya hivyo. Kupuuzwa kunaweza kueleweka kama ukosefu wa usawa na uwepo wa dhiki kwa muda mrefu inayotokana na ubaguzi, unyanyapaa wa kijamii na dhana potofu. Inaweza pia kufafanuliwa kama mchakato wa kijamii wa kuwa au kutupwa kwenye ukingo wa jamii. Kihistoria, baadhi ya vikundi vya kijamii vimekuwa havishirikishwi kwa sababu ya ubaguzi wa kijamii na kitamaduni, migogoro, uhamisho na uhamiaji. Makundi haya yaliyopuuzwa ni pamoja na wanawake, vijana, watu wenye ulemavu, watu waliokimbia makazi yao (IDPs), wakimbizi na wale walio ughaibuni. Katika miktadha mingine, vikundi vidogo

vya kikabila na kidini pia huangukia katika vikundi vilivyotengwa. EMBs zina jukumu la kuhakikisha kuwa makundi yaliyopuuzwa yanahimizwa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi kama wafanyakazi wa uchaguzi, wagombea au wapiga kura kwa kushughulikia mambo ambayo yanazuia ushiriki wao katika muhula wa uchaguzi. Mara nyingi, kanuni za uchaguzi hazijitoshelezi katika kuwa na vifungu ambavyo vinahimiza ushiriki katika uchaguzi wa makundi yaliyopuuzwa. Pale ambapo sheria ipo, utekelezaji umekuwa changamoto, kwa mfano, kuwezesha upigaji kura ughaibuni.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMBs zinapaswa kuwa na fasili pana ya ulemavu wa watu wenye ulemavu.
- EMBs zinapaswa kuzingatia usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa kijamii katika hatua mbalimbali za muhula wa uchaguzi kama vile usajili wa wapiga kura na wagombea, maandalizi ya kupigia kura, elimu ya wapiga kura, na kupiga kura.
- EMBs zinapaswa kutambua makundi yaliyopuuzwa nchini na kuendesha programu za kuelimisha wapiga kura ili kuondoa vikwazo vya ushiriki wao katika uchaguzi.
- Vyama vya siasa vinapaswa kuchukua hatua za upendeleo na juhudi nyingine mahsusi ambazo zinakuza uwakilishi wa makundi yaliyopuuzwa katika miundo ya vyama na katika uteuzi wa wagombea.

- EMBs inapaswa kuchukua hatua madhubuti na endelevu ili kufikia dhima ya ushiriki katika uchaguzi wa raia wanaoishi ughaibuni/kupiga kura nje ya nchi.
- Wadau wa uchaguzi wanapaswa kujitahidi kufanya lugha ya uchaguzi isiwe na ujinsia.

3.5 Ushiriki wa Asasi za Kiraia katika Uchaguzi

Kuunda asasi za kiraia ni sehemu muhimu katika mazingira ya kisiasa. Zinaweza kutetea na kukuza ujumuishaji katika mchakato wa uchaguzi na kutathmini utekelezaji wa muhula wa uchaguzi. Hata hivyo, katika baadhi ya nchi, Asasi za Kiraia (AZAKI) ni dhaifu na jukumu lao la uangalizi linakwamishwa na udhibiti wa serikali au ukosefu wa uwezo wa kitaasisi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Serikali inapaswa kutambua nafasi ya AZAKI na kuweka mfumo wezeshi wa kisheria ili kuwa huru katika kuhimiza ushiriki uchaguzi ulio mpana na jumuishi na pia kuwa na uwezo wa kutekeleza jukumu lao la uangalizi wakati wote wa zoezi la uchaguzi.
- EMBs zinapaswa kuidhinisha kwa wakati wasimamizi na waangalizi kutoka katika mashirika ya kiraia kutathmini awamu zote za uchaguzi.
- AZAKI zinapaswa kufanya shughuli zake kwa kufuata sheria husika za kitaifa na kanuni za uchaguzi.
- AZAKI zinapaswa kutathmini na kuripoti juu ya mchakato wa uchaguzi, kuendesha kampeni ya elimu ya mpiga kura, kuchangia katika kutambua na kupunguza mivutano inayojitokeza, kusaidia ujumuishaji na usalama wa jamii zilizopuuzwa (wanawake, vijana, na watu wenye

ulemavu) katika zoezi la uchaguzi, na kuhimiza mazingira ya uchaguzi wa amani.

- AZAKI pia zinapaswa kufuatilia na kuripoti mara kwa mara juu ya chama cha siasa na mgombea kufuata sheria ya uchaguzi, kanuni na taratibu za maadili.

3.6 Uteuzi na Usajili wa Wagombea

Kujidhatiti katika kuimarisha demokrasia lazima kuanze na demokrasia ndani ya chama. Zoezi la uteuzi wa wagombea ndani ya chama mara nyingi halifuati misingi ya kidemokrasia; kuna ukosefu wa mbinu za jumla za kukumbatia utofauti na uwakilishi sawa. Taratibu za uteuzi ndani ya vyama hazipaswi kusigina misingi ya kidemokrasia au uwakilishi wa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na makundi mengine yaliyosahaulika. Kuhusiana na mchakato wa uteuzi katika ngazi ya kitaifa, dukuduku lililopo katika baadhi ya nchi ni kutofikika kwa vituo vya uteuzi, hali ambayo wakati mwingine husababisha wagombea kuondolewa. Hata hivyo, baadhi ya EMBs zinafanya mchakato huu kidigitali na hivyo uteuzi wa mgombea unafanyika mtandaoni.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Mchakato wa uteuzi wa wagombea, wawe wa kujitegemea au wa chama, unapaswa kuwa wazi na wenye ratiba za kueleweka.
- Wagombea wanapaswa kuwasilisha fomu zao za uteuzi katika eneo la uchaguzi ambalo ni rahisi kwao kulifikia, kwa mfano, jimbo wanalogombea.
- Wagombea wanapaswa kuwa na muda wa kutosha wa kutekeleza matakwa ya mchakato wa uteuzi.

- Ada ya uteuzi inapaswa kuwa za kiungwana (ndogo) ili kuwezesha ushiriki mpana.
- Wagombea na wafanyakazi wa EMB wanapaswa kupewa ulinzi wa polisi wakati wa mchakato wa uteuzi na usajili.
- Kuwe na wakili au kamishna wa viapo katika kila wilaya na majimbo kurahisisha na kuharakisha upatikanaji na utekelezaji wa zoezi husika.
- Umma upewe muda wa kutosha kukagua orodha ya wagombea wateule ili kuweka pingamizi na migogoro kutatuliwa.
- Vyama vya siasa vinapaswa kuhamasisha wagombea wa kike na makundi mengine yaliyopuuzwa.
- Vyama vya siasa vinapaswa kuwa na wagombea wanawake ili kuhakikisha uwakilishi wa kijinsia unaendana na lengo la 50% ifikapo 2030, kama ilivyoainishwa katika Itifaki ya SADC iliyorekebishwa mwaka 2018 juu ya Jinsia na Maendeleo.

3.7 Kampeni

Kipindi kati ya mwisho wa uteuzi wa mgombea na siku ya uchaguzi hutumiwa na vyama vya siasa kufanya kampeni za kisiasa, ingawa kampeni zisizo rasmi kwa kawaida huanza mapema sana, ikiwa ni ukiukaji wa wazi wa sheria ya uchaguzi. Baadhi ya nchi za SADC, hata hivyo, hazitengi muda wa kutosha kwa ajili ya zoezi la uchaguzi. Katika kipindi cha kampeni, vyama shindani na wagombea hupuuza kanuni za

maadili na kufanya vitendo vinavyovunja sheria, kama vile kuweka 'zuio' kwenye baadhi ya maeneo, na hivyo kuzuia wapinzani kwenda maeneo hayo.

Sio vyama vyote vya siasa na wagombea wote hupata rasilimali za umma kwa ajili ya kampeni. Vyama tawala katika ukanda wa SADC hufaidika kinyemela katika eneo hili, hutumia rasilimali za umma ambazo huzisimamia kwa madhumuni ya kampeni au kuendeleza malengo yao ya kisiasa. Baadhi ya vyama na wagombea pia wanapata fedha za kibinafsi kutoka vyanzo vya ndani na vya kimataifa kwa ajili ya kuendeshea uchaguzi. Kutokana na kukosekana kwa kanuni juu ya ufadhili wa kampeni na ugumu wa kufuatilia matumizi ya fedha za kampeni, nchi nyingi zinakabiliwa na kuongezeka kwa ushawishi wa fedha kwenye siasa.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Lazima kuwe na kipindi cha kiungwana na kinachoeleweka cha kuanza rasmi na kumalizika kwa kampeni.
- Katika mchakato wa uchaguzi, vyama na wagombea wanapaswa kuzingatia kanuni za maadili ya uchaguzi ambazo zinaongoza mienendo yao na kusaini mkataba wa amani.
- Vyama vya siasa na wagombea wanapaswa kufadhiliwa kwa usawa na serikali kulingana na masharti yaliyowekwa.

- Matumizi ya mali za umma na fedha kutimiza malengo ya chama cha siasa yanapaswa kudhibitiwa ili kuwa na uwanja sawa wa ushindani wa kisiasa.
- Matumizi ya rasilimali za umma kwa ajili ya kampeni za kisiasa na shughuli za vyama vya siasa kwa ujumla yanapaswa kuepukwa, lakini, ikiwa inaruhusiwa, lazima zilipiwe na kutumiwa kwa sawa, na masharti ya upatikanaji wake na gharama husika lazima yawekwe wazi katika sheria.
- Vyama vya siasa na wagombea wanapaswa kuwajibika kwa EMB au chombo husika kwa matumizi ya rasilimali hizo.
- Polisi wanapaswa kutoa vibali vya mikutano rasmi na kutoa usalama kwa wagombea kwa namna isiyo na upendeleo.

3.8 Ushiriki wa Vyombo vya Habari katika Uchaguzi

Katiba nyingi za nchi za SADC zina uhuru wa vyombo vya habari kama haki ya msingi. Hata hivyo, katika nchi nyingi vyombo vya habari vya umma na vya kibinafsi vinaonekana kuwa na maslahi ya kisiasa. Mara nyingine, vyombo vya habari haviwajibiki vya kutosha kwa wananchi na vinahusika katika kuripoti kwa hisia na upendeleo. Hii ni kutokana na kukosekana kwa chombo madhubuti cha udhibiti wa vyombo vya habari.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Vyama vyote shindani na wagombea wanapaswa kupewa fursa (nafasi) sawa katika vyombo vya habari vya umma na vya kibinafsi, magazeti, elektroniki na mitandao ya kijamii.
- Kanuni za vyombo vya habari zinapaswa kutolewa na mamlaka huru ya vyombo vya habari inayohusika na kufuatilia na kusimamia vyombo vya habari kila siku.
- Kanuni zilizowekwa za vyombo vya habari zitumiwe na aina zote za mitandao ya kijamii.
- Uhabarishaji wa vyombo vya habari katika kipindi cha uchaguzi unapaswa kuongozwa na kanuni za maadili, mahsusi kwa ajili ya utoaji wa habari katika mizani ya haki na usawa.

- Vyombo vya habari vinapaswa kutoa kipaumbele kwa wagombea wanawake na wagombea wengine kutoka katika makundi yanayopuuzwa.
- Taarifa za vyombo vya habari zijiepushe na kuendeleza ujinsia na dhana nyingine potofu, na kusambaza taarifa danganyifu, za uongo na hotuba za chuki.
- EMBs zinapaswa kutoa mafunzo kwa vyombo vya habari juu ya mchakato wa uchaguzi na inapobidi kutoa vibali kwa vyombo vya habari kuripoti taarifa za uchaguzi.

3.9 Matumizi ya Intaneti na Mitandao ya Kijamii

Kiwango cha matumizi ya Intaneti na simujanja katika ukanda huu kiko juu, na kufanya matumizi ya majukwaa ya mitandao ya kijamii kama vile Facebook, WhatsApp na Twitter kuenea. EMBs hutumia majukwaa na tovuti hizi kwa ajili ya kuelimisha na kutoa taarifa kwa mpiga kura. Vyama vya siasa hushiriki katika zoezi la uchaguzi kupitia mitandao ya kijamii na kusambaza taarifa kwa umma ulioko mitandaoni ndani ya muda mfupi. AZAKI hutumia majukwaa haya kuhamasisha ushiriki katika uchaguzi na uchaguzi wa amani. Wakati huo huo, wapiga kura wanashiriki katika mijadala na mazungumzo ya kisiasa kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii.

Vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi wanafurahia uhuru mkubwa wa kujieleza kwenye Intaneti na mitandao ya kijamii ikilinganishwa na vyombo vya habari vya jadi ambavyo vinasimamiwa zaidi. Kwa kuongezea, mitandao ya kijamii inakuza upatikanaji wa habari na ushiriki wa raia katika siasa, na hivyo kukuza demokrasia ya dijitali.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMBs na mashirika husika ya serikali, yanayofanya kazi kwa kushirikiana na majukwaa ya mitandao ya kijamii, wanapaswa kutumia zana zilizopo kufuatilia kampeni na shughuli za kisiasa kwenye mitandao ya kijamii kipindi cha uchaguzi.
- Mashirika ya ufuatiliaji wa vyombo vya habari yanapaswa pia kufanya ufuatiliaji wa mitandao ya kijamii.
- EMBs zinapaswa kuendaa miongozo ya mitandao ya kijamii na kushirikisha makampuni ya teknolojia na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha kuwa uchaguzi unafanyika katika mazingira yenye taarifa zinazoaminika na kwamba majukwaa yao hayatumiwi kudhoofisha kuaminika kwa uchaguzi.

3.10 Upotoshaji wa Habari na Hotuba za Chuki;

Matumizi makubwa ya mitandao ya kijamii na kasi ambayo habari husambaa mtandaoni imesababisha ukuaji wa habari potofu, habari za uongo na propaganda, ambazo kwa kawaida hujulikana kama 'habari bandia'. Habari hizi huenea kupitia simulizi zilizotiwa chumvi, vichwa vya habari vya kupotosha, taarifa za habari za upendeleo na ukweli unaowasilishwa nje ya muktadha wake. Habari bandia zinawasilishwa ili kupotosha kwa makusudi, kuchochea mvutano na kuleta hali ya kutoaminiana. Pia hutumiwa kueneza hotuba za chuki, kuchafua sifa, na kudhoofisha imani ya wananchi katika Chombo Kinachosimamia Uchaguzi. Kwa namna hii, mitandao ya kijamii imekuwa ni uwanja wa kudanganya wapiga kura na

kuendesha kampeni chafu na za mgawanyiko, na kutishia uvunjifu wa haki za binadamu na demokrasia.

Kutokomeza taarifa potofu na hotuba za chuki mtandaoni bado ni changamoto. Baadhi ya majukwaa kama vile Facebook na Twitter yanaweza kuzuia akaunti zinazoeneza habari bandia na maudhui yasiyofaa, lakini mfumo wa usimbaji fiche wa WhatsApp unafanya zoezi hili kuwa gumu. Utaratibu wa kujiridhisha juu ya ukweli wa taarifa unaofanywa na majukwaa ya mitandao ya kijamii na mashirika ya habari ni njia nzuri ya kutokomeza habari bandia. Hata hivyo, jitihada hizi zinaathiriwa na kufifia kwa ubora wa vyombo vya habari na uandishi duni wa habari.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Wanasiasa lazima wajiepushe na kampeni hasi na kuwazua wafuasi wao wasizalishe na kueneza habari bandia na maudhui yenye madhara kwenye mitandao ya kijamii.
- Kanuni za maadili kwa vyama vya siasa zinapaswa kujumuisha kifungu kinachopiga marufuku kampeni za chuki, taarifa potofu na taarifa za uongo.
- Sheria za usimamizi wa vyama vya siasa zinapaswa kujumuisha vifungu vinavyodhibiti shughuli za mtandaoni za vyama, wagombea na wafuasi wao.
- EMB na AZAKI zinapaswa kutoa elimu ya uraia ili kuwawezesha wananchi kutambua, kuripoti na kukabiliana na habari bandia.

- Vyama vya siasa na wagombea wanapaswa kuhakikisha ujumbe na habari wanazotoa ni za kweli na sahihi.
- Kutokana na kuwa na jukumu muhimu katika jamii, EMBs zinapaswa kuhamasisha mashirika ya vyombo vya habari kuboresha utoaji taarifa za uchaguzi, hili linaweza kufanikiwa kwa kuwafikia wananchi na kutoa elimu kabambe ya uraia. Wanapaswa pia kufuatilia ukweli na habari bandia katika mitandao ya kijamii.
- Umma kwa ujumla unapaswa kujiepusha kuzalisha na kueneza habari bandia na maudhui yenye madhara kwenye mitandao ya kijamii.

3.11 Vurugu za Kisiasa

Kunaweza tu kuwa na mchakato wa uchaguzi ambao ni huru, wa haki, wa kuaminika na halali katika mazingira ambayo hayana vurugu za kisiasa na vitisho. Hata hivyo, vurugu za kisiasa zinazohusiana na uchaguzi na vitisho vya wafuasi wa chama zimetokea ikiwa ni pamoja na kuwalenga wagombea wanawake na wanawake katika maisha ya kawaida. Kwa hiyo, kuna haja ya kujenga utamaduni wa amani na uvumilivu, na kukubaliana kwa ujumla juu ya tabia zinazokubalika na zisizokubalika.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Wadau wote wa uchaguzi wanapaswa kujitolea kukuza na kueneza utamaduni wa amani na uvumilivu kabla ya, wakati wa, na baada ya siku ya uchaguzi.

- Kanuni za maadili zinazodhibiti tabia za vyama vya siasa na wafuasi wao zinapaswa kupitishwa kupitia mchakato wa mashauriano unaohusisha EMB, vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi.
- Vyama vya siasa na vikosi vya usalama vinapaswa kushirikiana na kuhakikisha usalama wa wagombea, hasa wagombea wanawake.

4. Kipindi cha Uchaguzi

4.1 Hatua za Kiusalama

Jukumu la vikosi vya usalama vya serikali – jeshi, polisi na ujasusi – katika kulinda mchakato wa uchaguzi halijazingatiwa vizuri katika nchi za SADC. Kwa kawaida, ni polisi ambao husimamia sheria na utulivu kila siku, ikiwa ni pamoja na siku ya uchaguzi na kuhesabu kura. Katika baadhi ya maeneo, uwepo wa vikosi vya usalama karibu na vituo vya kupigia kura kunaweza kuwatisha na kuwatia hofu wapiga kura. Hata hivyo, polisi wana jukumu muhimu katika kulinda vifaa vya uchaguzi, wafanyakazi wa uchaguzi na wapiga kura dhidi ya vitisho na kwa hivyo wanapaswa kuwa katika vituo vya kupigia kura na vituo vya matokeo. Baadhi ya nchi zimekumbwa na uharibifu wa vifaa vya uchaguzi na wafanyakazi wa uchaguzi wametishwa na kuumizwa.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Vikosi vya usalama vinapaswa kufundishwa namna ya kulinda uchaguzi na kutopendelea upande wowote katika kulinda uchaguzi.
- Vikosi vya usalama vinapaswa kudhibitiwa na kanuni za maadili zilizomo katika sheria ya uchaguzi na hulka zao hazipaswi kuwatisha wapiga kura.
- EMB inapaswa kukutana mara kwa mara na vikosi vya usalama kujadili masuala yanayohusiana na kulinda nyenzo na vifaa vya uchaguzi, wafanyakazi wa uchaguzi, usalama wa siku ya kupigia kura, usalama wa kitaifa wakati wa uchaguzi, na kutoa msaada

mwingine wowote wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu ambao unaweza kuhitajika katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi.

- Sheria maalum inapaswa kutungwa kuruhusu vikosi vya usalama kupiga kura siku moja kabla ya Siku ya Uchaguzi ikiwa watapangiwa kazi mbali na majimbo yao.

4.2 Nyenzo na Vifaa vya Kupigia Kura

Nchi nyingi za wanachama wa SADC, ikiwa ni pamoja na zile ambazo zina mifumo ya kupiga kura ya kielektroniki, hutumia karatasi za kura na masanduku ya kura. Mara nyingi, EMB inasimamia uzalishaji na usalama wa vifaa vya kupigia kura. Katika hali nyingi, vifaa nyeti vya uchaguzi huchapishwa nje ya nchi kwa sababu ya ukosefu wa imani kwa wachapishaji wa ndani. Ikiwa haitashughulikiwa vizuri na EMB, ununuzi, usambazaji na aina za vifaa vya uchaguzi vinaweza kusababisha mgogoro.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Karatasi za kupigia kura zinapaswa kusanifiwa na kuchapishwa chini ya udhibiti na usimamizi wa EMB pekee na chini ya ulinzi madhubuti.
- Usanifu wa vifaa vyote vya uchaguzi unapaswa kufanana.
- Vifaa vyote vya uchaguzi vinapaswa kusambazwa kwenye vituo vyote vya kupigia kura kwa wakati na kiwango cha kutosha.
- Vifaa vya uchaguzi vinapaswa kununuliwa kwa njia ya uwazi na kwa mujibu wa sheria.
- Karatasi za kupigia kura zinapaswa kusanifiwa kwa namna ambayo ni ya kirafiki na wapiga kura wanaweza kuieleweka kirahisi.
- Jitihada zinapaswa kufanywa kusanifu vifaa vya uchaguzi ambavyo ni rahisi kutumiwa na wapiga kura wasiojiweza kama vile vipofu na viziwi. Ikiwa hakuna vifaa hivi, msaada unapaswa kutolewa ili kuwawezesha wapiga kura hao kupiga kura.
- Vifaa nyeti vya uchaguzi vinapaswa kuhifadhiwa na kutolewa chini ya ulinzi mkali ili kuzuia udanganyifu (wizi) wa kura.
- Katika mazingira ambayo vifaa nyeti vya uchaguzi vinapaswa kuhifadhiwa kwa usiku mmoja, mawakala wa vyama na waangalizi wanapaswa kuruhusiwa kubaki kwenye kituo cha kupigia kura chenye vifaa husika.

4.3 Maeneo ya kupigia kura

Kuongeza ushiriki wa wananchi katika mchakato wa uchaguzi ni njia muhimu ya kuimarisha demokrasia. Lengo hili linaweza kufikiwa ikiwa tu umma una imani na mchakato wa uchaguzi na ikiwa vituo husika vinafikika. Kukosa imani na vituo kutofikika vizuri kunaweza kusababisha wapiga kura kutojali, kama inavyoonekana kwa baadhi ya nchi ambapo idadi ndogo ya wapiga kura hujitokeza.

Sehemu ambapo vituo vya kupigia kura vinawekwa ina changia sana katika mchakato kufikika. Uwepo wa vituo vya kupigia kura mahali, kwa kawaida, hutegemea mambo kadhaa kama vile idadi ya wapiga kura kwa kila kituo, ukaribu wa kituo kwa wapiga kura, utoshelevu wa mwanga na mawasiliano, usafiri na masuala mengine ya ugavi.

Katika nchi nyingi wanachama wa SADC, hakuna usawa kati ya miundombinu na huduma katika maeneo ya mijini na vijijini. Vituo vya kupigia kura katika maeneo ya mijini huwa vinafikika kwa urahisi na kuhudumiwa vizuri ukilinganisha na majimbo ya vijijini.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Pale inapowezekana, mipango maalum inapaswa kufanywa ili kuruhusu makundi maalum ya wapiga kura, kama vile wapiga kura wanaoishi nje ya nchi na wafungwa, kupiga kura.
- Sheria inapaswa kuruhusu upigaji kura maalum au mapema kwa polisi, wafanyikazi wa uchaguzi na wafanyikazi wa huduma muhimu ambao watafanya kazi siku ya uchaguzi.
- Kumbi zinazotumiwa kama vituo vya kupigia kura zinapaswa kuwa katika maeneo ambayo yanafikika kwa wapiga kura wote, hasa wazee na watu wenye ulemavu. Mipango ya dharura inapaswa kuwekwa ili kujidhatiti na hali mbaya ya hewa au isiyotarajiwa.
- Kunapaswa kuwa na vituo vingi vya kupigia kura kuendana na idadi ya watu na mpangilio wa makazi ili kufikika kirahisi, kupunguza muda wa kusubiri na kuongeza ufanisi.
- Vituo vya umma vyenye miundombinu muhimu, kama vile shule, vinapaswa kupewa kipaumbele kama vituo vya kupigia kura.
- Pale ambapo miundombinu ni finyu, kuwe na utoaji wa kutosha wa njia mbadala. Ikiwa ni lazima, vifaa vinavyotembea (vinavyohamishika) vinapaswa kutumiwa.

4.4 Wasimamizi wa Uchaguzi

Chaguzi hutumia nguvu kazi kubwa, hivyo kuhitaji kuajiri na kutoa mafunzo kwa maelfu ya wafanyakazi wa muda ambao wanasambazwa nchi nzima kabla ya kupiga kura. Katika siku ya uchaguzi, jukumu lao ni kuwezesha mchakato wa kupiga kura. Idadi ya wafanyakazi kwa kila kituo cha kupigia kura imeainishwa katika miongozo ya uchaguzi iliyotolewa na EMBs. Kutokana na muda mrefu wa saa za kazi siku ya kupiga kura na kazi husika inavyochosha, EMB inahitaji kuhakikisha kuwa wana wafanyakazi wa kutosha kufanya kazi iliyopo kwa zamu na kwamba ustawi wa wasimamizi wa uchaguzi unazingatiwa.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMB inapaswa kutaasisisha vigezo vya kuajiri (kuteua) wasimamizi wa uchaguzi na michakato ya kusimamia utendaji wao.
- Wasimamizi wa uchaguzi wanapaswa kuajiriwa na EMB kwa njia ya uwazi na isiyo na upendeleo wa kisiasa.

- Katika kuajiri wasimamizi wa uchaguzi ni muhimu kuzingatia usawa wa kijinsia na uwakilishi wa makundi yaliyopuuzwa.
- Wasimamizi wa uchaguzi wanapaswa kuajiriwa mahali wanapoishi, kwa kadri inavyowezekana.
- Wasimamizi wa uchaguzi hawapaswi kunyimwa haki ya kupiga kura na hivyo wanapaswa kuwa na uwezo wa kupiga kura katika vituo vyao vya kazi. Vinginevyo, EMB inapaswa kuhakikisha kuwa maafisa ambao watakuwa wakifanya kazi katika vituo vya kupigia kura tofauti na mahali walipojiandikisha wanaweza kupiga kura mapema.
- EMB inapaswa kuandaa miongozo ya wasimamizi wa uchaguzi na kuwafundisha vizuri kabla ya siku ya uchaguzi.
- EMB inapaswa kuweka sawa masuala yote ya ugavi na usafirishaji wasimamizi wa uchaguzi na kuwapa utambulisho wa wazi.
- Mawakala wa vyama, waangalizi na watu wowote walioidhinishwa kuwepo katika kituo cha kupigia kura wanapaswa kufuata taratibu bila kuingilia majukumu ya wasimamizi wa uchaguzi au kuwatisha.
- EMB inapaswa kuhakikisha kuwa kuna ulinzi wa kutosha kulinda wasimamizi wa uchaguzi.
- Wasimamizi wa uchaguzi wanapaswa kutia sahihi kufuata kanuni za maadili.

- Wasimamizi wa uchaguzi wanapaswa kufuata taratibu zote za kupiga kura zilizowekwa kama vile kufungua na kufunga zoezi la upigaji kura, kuhesabu na kutuma (kubandika) matokeo.

4.5 Taratibu za Upigaji Kura

Taratibu za upigaji kura zimewekwa katika kanuni za uchaguzi na lazima zifuatwe siku ya kupiga kura. Wapiga kura lazima wahakikishe kuwa wanafika kwenye kituo cha kupigia kura ambako wamejiandikisha kupiga kura na wamebeba kitambulisho cha mpiga kura. Wasimamizi wa uchaguzi wanatakiwa kuzingatia taratibu za ufunguzi, kuandaa kituo cha kupigia kura, kutambua wapiga kura kwenye daftari husika, kutoa karatasi za kupigia kura, kupaka wapiga kura wino, kusaidia makundi ya wapiga kura ambao yanahitaji msaada, kushughulikia malalamiko na kuzingatia taratibu za kufunga uchaguzi. Baada ya kumaliza zoezi la kupigia kura, wasimamizi wa uchaguzi wanawajibu kulinganisha kura, kuhesabu kura, kubandika matokeo yaliyosainiwa katika kituo cha kupigia kura na kupeleka (kutuma) matokeo husika kwenye kituo cha kukusanyia matokeo kama sheria inavyotaka.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Wakati wa ufunguzi na kufunga zoezi la upigaji kura, taratibu za kushughulikia, kufunga na kuweka chapa ya usalama kwenye masanduku ya kura linapaswa kuwa wazi na kukaguliwa na mawakala wa chama, waangalizi, na wadau wengine walioidhinishwa ambao wanaweza kuwapo.

- Vituo vya kupigia kura vinapaswa kupangwa ipasavyo ili kuhakikisha vinafikika kirahisi, vinapitika vizuri na vinazingatia usiri wa kura.

- Wasimamizi wa uchaguzi wanapaswa kutoa fursa ya upendeleo kwa wazee, wanawake wajawazito, watu wenye ulemavu na wapiga kura wengine wenye mahitaji maalum kwa mjibu wa sheria.

- Mbinu zinazofaa zinapaswa kuwekwa ili kuzuia upigaji kura mara nyingi.
- Ikiwa kuna matumizi ya mashine za kupigia kura:
    - taratibu zinapaswa kuwapo ili kuhakikisha kuwa mashine zote za kupigia kura zitakazotumika katika vituo vya kupigia kura hazina kura zozote;
    - mawakala wote wanapaswa kuruhusiwa kukagua mashine za kupigia kura;
    - kunapaswa kuwa na taratibu zinazohakikisha kuwa mashine zote za kupigia kura zimefungwa utepe wa siri mwanzoni na mwishoni mwa zoezi la kupiga kura kwa njia iliyoamuriwa;
    - mashine zinapaswa kutumiwa pamoja na mfumo mahsusi wa kukagua na kuthibitisha mpiga kura; na
    - vifaa husika vinapaswa kuwa rahisi kuvitumia.

4.6 Usiri wa Kura

Usiri wa kura ni moja ya nguzo muhimu za uchaguzi ambao ni huru, wa haki, wa kuaminika na halali. Ili kuepuka kutuhumiana, kutoaminiana, vurugu za kisiasa, vitisho na hofu ya kulipiza kisasi cha kisiasa na kuteswa kwa wapiga kura, maafisa wa uchaguzi, mawakala wa vyama na wafuasi wa vyama wanahitaji kuhakikishiwa kwamba watapiga kura ya siri.

Nchi nyingi wanachama wa SADC zinazingatia usiri wa kura. Hata hivyo, kumekuwa na visa ambapo majaribio ya

kudhoofisha usiri wa kura kupitia taarifa potofu na vitisho yameripotiwa.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Kituo cha kupigia kura kinapaswa kupangiliwa kwa namna ambayo hakuna mtu anayeweza kuona jinsi wapiga kura wanavyochagua au kuweka alama kwenye karatasi zao za kupigia kura au mashine ya kupigia kura.
- Lazima kuwe na utaratibu mzuri wa utoaji msaada muhimu kwa watu wenye ulemavu, wapiga kura wasiojua kusoma na kuandika na wazee, na ambao hulinda, kwa kadri inavyowezekana, haki yao ya kupiga kura kwa siri.
- Pale ambapo karatasi za kupigia kura zimebuniwa kwa kutumia mashina (vibutu) na mfuatano wa namba,

tahadhari zote zinapaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa haiwezekani kuoanisha kura zilizopigwa na majina ya wapiga kura husika, kwa mfano, kwa kujaza namba zao za utambulisho kwenye kishina (kibutu).

- Wapiga kura wasiruhusiwe kutumia kamera ndani ya kibanda cha kupigia kura, ama kwa kupiga picha au kuchukua video ya karatasi ya kupigia kura iliyowekwa alama.
- Ni marifuku kwa mtu asiyehusika kuondoa karatasi ya kupigia kura kutoka kwenye chumba cha kupigia au kuhesabu kura au kukutwa na karatasi husika.

4.7 Wakala wa Chama/Wagombea

Chama cha siasa na mawakala wa wagombea waliotambuliwa wana haki ya kuwepo katika vituo vya kupigia na kuhesabu kura. Jukumu lao ni kufuatilia mchakato wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kuhesabu na kukusanya kura. Uwepo wao unalenga kuwa na uchaguzi wa wazi na amani.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMB inapaswa kuidhinisha mawakala kwa wakati.
- Vyama vya siasa na wagombea binafsi lazima wahakikishe kuwa mawakala wao wamefundishwa juu ya mfumo wa uchaguzi, haki, majukumu, na wajibu.
- Vyama na wagombea binafsi wanapaswa kushughulikia kikamilifu masuala yote yanayohusu ugavi na usafirishaji wa mawakala wao.
- Lazima kuwe na kanuni za maadili kwa mawakala wa chama na mgombea.

- Wagombea wanapaswa pia kuajiri mawakala wanawake ili kukuza uwakilishi wa kijinsia.
- Mawakala wanapaswa kuwa na nakala ya daftari la wapiga kura katika siku ya uchaguzi na orodha ya kupimia (kukagulia) yao wenyewe.
- Mawakala wanapaswa kusambazwa katika vituo vingi vya kupigia kura kwa kadri inavyowezekana.
- Mawakala wanapaswa kusaini na kupewa nakala ya karatasi ya matokeo ya kituo cha kupigia kura.

5. Usimamizi wa Matokeo

5.1 Kuhesabu kura na Usimamizi wa Matokeo

Kuhesabu kura huanza katika kituo cha kupigia kura na hufanywa kwa mikono au kidijitali ikiwa mashine za kupigia kura zimetumika. Alama huingizwa katika fomu husika na nakala hubandikwa mahali panapoonekana katika sehemu (kitengo) ya kuhesabia kura. Usafirishaji wa kura kati ya vituo vya kupigia na kuhesabia kura ni chanzo cha kutuhumiana na udanganyifu na lazima ishughulikiwe kwa ulinzi wa hali ya juu na uwazi. Karatasi halisi za matokeo (kura) hubebwa kiuhalisia na/au kutumwa kwa njia ya mtandao na kupelekwa kwenye vituo vilivyotengwa kwa ajili ya kulinganisha (kupanga) na kutangaza matokeo. Ili kuongeza uaminifu na uwazi katika zoezi la kuhesabu kura, nchi kadhaa za SADC zimeanzisha vituo mahsusi vya matokeo na hutumia teknolojia ili kutoa takwimu za matokeo kitaifa.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMB inapaswa kuwa na jukumu la jumla la kuhesabu kura na usimamizi wa matokeo.
- Maafisa uchaguzi, mawakala wa vyama/wagombea, waangalizi na watu wengine walioidhinishwa na ambao wanaruhusiwa kuwepo wakati wa zoezi la kuhesabu kura wanapaswa kujuzwa taratibu za kuhesabu.
- Mchakato wa kuhesabu kura unapaswa kufanyika katika kituo cha kupigia kura mara tu baada ya kufungwa kwa zoezi la upigaji kura.

- Ili kituo cha kupigia kura kifanye kazi kwa ufanisi kama kituo cha kuhesabia, lazima kiwe na taa (mwanga) za kutosha, hewa safi (salama), ulinzi na mifumo ya mawasiliano, pale inapowezekana.
- Mawakala wa vyama vya siasa na wagombea wanapaswa kusaini karatasi za matokeo pindi tu mchakato wa kuhesabu kura utakapokamilika.
- Matokeo yatangazwe mara moja na kubandikwa katika kituo cha kupigia kura.
- Pale inapowezekana, mfumo wa sheria unapaswa kutoa miongozo ya wazi juu ya utumaji (utangazaji) wa matokeo kwa njia ya mtandao.
- Ikiwa kuna utumaji (utangazaji) wa matokeo kwa njia ya mtandao, wasimamizi wa uchaguzi lazima wawe na vitendea kazi husika na wapate huduma ya Intaneti thabiti.

5.2 Utangazaji wa Matokeo ya Jumla

Katika nchi nyingi za SADC, EMB ina jukumu la kutangaza matokeo rasmi ya uchaguzi. Ni kawaida matokeo kuchelewa sana kutangazwa kwa sababu ya kasi ndogo katika upangaji matokeo, miundombinu duni na uratibu mbovu wa zoezi zima. Hali hii husababisha wasiwasi na kupunguza uwezekano wa kukubali matokeo, yote haya yanaondoa imani katika mfumo wa uchaguzi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Vituo mahsusi vya matokeo vinapaswa kuanzishwa katika nchi zote za SADC na vinapaswa kuwa wazi kwa watu waliotambuliwa na kuidhinishwa rasmi ili

kuzidisha uwezekano wa matokeo ya uchaguzi kukubalika.

- Sheria ya uchaguzi inapaswa kuweka muda maalum ambao matokeo lazima yatangazwe, ili kupunguza mashaka na migogoro au udanganyifu unaoweza kujitokeza.
- Sheria za uchaguzi zinapaswa kuonyesha wazi ni taasisi ipi yenye mamlaka ya kisheria kutangaza matokeo.
- Matokeo kutoka vituo vya matokeo yanapaswa kutangazwa na kubandikwa sehemu ya umma, papohapo na mara kwa mara.
- Muda muafaka unapaswa kuwekwa kwa ajili ya uthibitisho wa matokeo na ugawaji wa viti (vya uwakilishi).
- Ripoti ya uchaguzi ya EMB inapaswa kuonesha na kuchanganua kiundani idadi ya wapiga kura wanaostahili (waliojiandikisha) na idadi ya wapiga kura waliopiga kura.
- EMB inapaswa kuchapisha kwa wakati matokeo ya kina ya uchaguzi kwenye tovuti yake.
-

6. Baada ya Uchaguzi

6.1 Migogoro Baada ya Uchaguzi

Katika baadhi ya nchi za SADC, matokeo ya uchaguzi yamepingwa kwa sababu mbalimbali ambazo ni pamoja na kutoridhika na mwenendo wa EMB katika kusimamia uchaguzi. Hii huibua hisia za kukosekana uwazi na uwajibikaji, na kutoridhishwa na mfumo wa 'mshindi-kuchukua-vyote', ambao huibua hisia za kuenguliwa katika mchakato husika.

Migogoro baada ya uchaguzi huibuka katika uchaguzi wenye ushindani mkubwa ambapo washindani huamini wameshinda na hivyo kukataa matokeo. Kwa hivyo, ni muhimu sana kuwekwa utaratibu ili kukabiliana na migogoro ya namna hii kwani inaweza kudhoofisha uaminifu katika mchakato wa uchaguzi na kusababisha mgogoro wa kijamii ama wa wazi au siri.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Ni muhimu kujenga utamaduni wa kukubali matokeo ya uchaguzi kupitia elimu ya uraia na kukuza utaratibu wa kufanya uchaguzi wa uwazi.
- Lazima kuwe na vifungu vya wazi vya kisheria vinavyotoa haki ya kukata rufaa dhidi ya matokeo na mambo mengine yoyote yanayohusiana na mwenendo wa uchaguzi.
- Muundo wa kitaasisi wowote wa utatuzi wa migogoro ulioanzishwa, ukisaidiwa na njia nyingine sahihi za kimamlaka, vinapaswa kuhuishwa baada ya uchaguzi ili kusaidia utatuzi wa migogoro.

- Mfumo wa sheria unapaswa kuweka wazi muda wa kufungua na utatuzi wa kesi za maombi na mashauri ya uchaguzi.

6.2 Marejeleo na Tathmini ya Baada ya Uchaguzi

Kuendesha uchaguzi unaoaminika, wenye gharama nafuu na endelevu kunahitaji kufanyika kwa tathmini baada ya uchaguzi, ama kwa njia ya tathmini ya washauri waelekezi - waliokubaliwa na EMB, au kwa kutumia kura za maoni, kupata mtazamo wa mpiga kura baada tu ya kupiga kura, na kufanya utafiti. Katika nchi nyingi za SADC, EMBs hufanya tathmini baada ya uchaguzi. Hata hivyo, zoezi la tathmini baada ya uchaguzi huwatenga wadau muhimu mara kadhaa, wakati hufanywa kwa nia ya kuboresha mwenendo wa chaguzi zijazo. Pamoja na mapendekezo ya makundi ya waangalizi wa uchaguzi, tathmini hizi huibua ajenda ya kufanya mageuzi ya mfumo wa uchaguzi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- Ili kutathmini mchakato husika kwa ufanisi, ni muhimu kujumuisha katika tathmini wadau wa uchaguzi kama vile Makamishna na wafanyakazi wa EMB, vyombo vya usalama na mashirika husika ya serikali, vyama vya siasa, Wabunge, waangalizi, vyombo vya habari, wafadhili na AZAKI.

- Takwimu za upigaji kura zijumuishwe kwenye tathmini, zioneshe ni wanawake, wanaume na vijana wangapi wenye umri tofauti waliopiga kura. Hii inatoa taarifa muhimu (taswira) kwa mipango ya baadaye ya uchaguzi na elimu ya wapiga kura.

- Wadau wa uchaguzi wanapaswa kujuzwa matokeo ya mchakato wa tathmini.
- EMB inapaswa kuwasilisha ripoti ya mwisho juu ya uchaguzi kwa taasisi husika.
- EOMs zinapaswa kuwasilisha kwa wakati ripoti zao za mwisho kwa EMB, na kubainisha maeneo yanayopaswa kuboreshwa na kufanyiwa marekebisho ya kisheria.
- EMB inapaswa kufanyiwa tathmini kila baada ya uchaguzi.

7. Ufuatiliaji na Uangalizi wa Uchaguzi

7.1 Mawanda na Methodolojia/Mbinu

Ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi umekuwa sehemu muhimu ya mchakato wa uchaguzi katika nchi za SADC, huku nyingi zake zikikubali wafuatiliaji/waangalizi kutoka mashirika ya kimataifa, kikanda na kitaifa. Wafuatiliaji/waangalizi hao wanatarajiwa kuwa na jukumu muhimu katika kuimarisha uwazi na kuaminika kwa uchaguzi na kukubalika kwa matokeo.

Ingawa maneno 'ufuatiliaji' na 'uangalizi' mara nyingi hutumiwa kwa kubadilishana, ni muhimu kuzingatia kwamba mifumo hii miwili, kwa kweli, ni tofauti, licha ya kuunganishwa. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Umoja wa Afrika wa Uangalizi na Ufuatiliaji wa Uchaguzi (2002), uangalizi unamaanisha kukusanya taarifa na kufanya uamuzi sahihi, wakati ufuatiliaji unahusisha kuangalia mchakato wa uchaguzi ukiwa na mamlaka ya kuingilia kati katika mchakato ikiwa sheria husika au taratibu za kawaida zinakiukwa au dharaulika. Pia, Miongozi hiyo hiyo ya AU inafafanua 'tathmini ya uchaguzi' kama tathmini ya awali ya mazingira ambayo uchaguzi utafanyika, itolewayo papo hapo.

Ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi unaweza kuwa wa aina mbili kuu: (a) wa muda mrefu, hujikita katika awamu zote za mchakato wa uchaguzi; na (b) wa muda mfupi, hujikita katika siku za mwisho za kampeni na matukio ya siku ya kupigia kura. Mifumo hii ni nyenzo muhimu za kutathmini na kuamua kama mchakato wa uchaguzi katika nchi yoyote umefanywa kwa njia huru, ya haki, ya uwazi na ya kuaminika au la. Kwa kuongezea, ufuatiliaji na uangalizi unaweza kusaidia nchi inayofanya

uchaguzi kuzuia, kutatua na/au kukabili migogoro inayohusiana na uchaguzi kwa kutoa taarifa bila upendeleo na kwa wakati, pamoja na kutambua ubora na udhaifu unaoweza kulikumba zoezi zima la uchaguzi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- EMB au mamlaka husika lazima ialike misheni za uangalizi kwa wakati ili kuruhusu misheni kujiandaa vya kutosha.
- EMB lazima ihakikishe kuwa mchakato wa kutambua (kuteua) waangalizi na wafuatiliaji unafanyika kwa haraka, ni fanisi na hauna ubaguzi.
- Baada ya kutambuliwa, wafuatiliaji na waangalizi wanapaswa kupewa ulinzi sawa kisheria na mamlaka za nchi kama raia yeyote wa nchi mwenyeji.
- EMB inapaswa, kwa kushauriana na wadau muhimu wa uchaguzi, kuandaa kanuni za maadili kwa wafuatiliaji na waangalizi wa uchaguzi ili kuhakikisha

mwenendo (tabia) unaokubalika, kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi inayofanya uchaguzi.

- Ni muhimu kwamba kanuni husika za maadili zisiwabane wafuatiliaji na waangalizi kwa namna ambayo wanashindwa kutekeleza majukumu yao kwa uhuru.
- Ufuatiliaji/uangalizi wa uchaguzi unapaswa kuzingatia kanuni za maadili zilizotungwa na EMB ya nchi mwenyeji. Kanuni za msingi zinazosimamia maadili ya wafuatiliaji/waangalizi wa uchaguzi zinapaswa kuangazia mienendo (tabia) yao kwa kuzingatia tunu zifuatazo, kati ya nyingine nyingi:
  - kufuata katiba na sheria za nchi mwenyeji;
  - kuheshimu tamaduni na mila za nchi mwenyeji;
  - kutangaza mgongano wowote wa kimaslahi kabla ya kushiriki katika misheni;
  - kutenda kwa namna isiyo na upendeleo wala mlengo fulani kuhusiana na wadau wote wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na wapiga kura, vyama vya siasa au wagombea, na vyombo vya habari;
  - kujiepusha na vitendo ambavyo vinaweza kuchukuliwa kuwa wanaonesha huruma kwa mgombea fulani au chama cha siasa;
  - kutovaa alama (nembo) yoyote ya chama au rangi;

- kuchangia kuhalalisha au vinginevyo mchakato wa uchaguzi na matokeo yake;
- kusaidia kuimarisha na kuheshimu haki za msingi za kisiasa, kijamii, kisheria na haki nyingine za binadamu katika nchi mwenyeji;
- kuongeza imani ya raia katika mchakato wa uchaguzi;
- kusaidia na kuonesha kujali kwa wale wanaohusika moja kwa moja na mchakato wa uchaguzi;
- kufunua na kuweka hadharani ukiukwaji (makosa) na kasoro zozote walizoziona katika mchakato wa uchaguzi ili ziweze kurekebishwa na taasisi husika; na
- kufanya uamuzi sahihi na kutumia kiwango cha juu cha utashi binafsi wakati wote.

- Kwa kadiri inavyowezekana, misheni za ufuatiliaji na uangalizi zinapaswa kupeleka timu ya kufanya tathmini kabla ya uchaguzi kwenye nchi mwenyeji miezi kadhaa kabla ya siku ya kupiga kura ili kujua kama kuna masharti ya msingi au la kabla ya kutuma misheni husika. Masharti haya ni pamoja na shughuli za kisiasa kufanyika kwa uhuru na kuhakikishiwa kwamba wafuatiliaji na waangalizi wanaweza kuzunguka kwa uhuru na kushirikiana na mashirika yoyote watakayochagua ili kuwasaidia katika kufanya tathmini ya mchakato wa uchaguzi.
- Misheni za ufuatiliaji na uangalizi zinapaswa kujiandaa kwa wakati na kikamilifu kwa ajili ya uangalizi na ufuatiliaji wa uchaguzi ili kuweka vizuri mipango yao ya

ugavi na usafirishaji kabla ya siku ya kupiga kura. Tathmini zao zinapaswa kugusa hatua nyingi za msimu wa uchaguzi kwa kadri inavyowezekana.

- Misheni za ufuatiliaji na uangalizi lazima zikusanye na kuwapatia waangalizi wao kabrasha lenye nyaraka muhimu zinazoelezea kwa ufupi mazingira ya kisiasa, mfumo wa kisheria, usalama, maeneo yao ya kazi, mbinu, kuripoti na taarifa nyingine zozote muhimu kwa ajili ya kutathmini zoezi la uchaguzi.
- Misheni za ufuatiliaji na uangalizi zinashauriwa kutatua changamoto kwa teknolojia ili kuleta ufanisi katika mchakato wa uangalizi.
- Misheni za ufuatiliaji na uangalizi zinapaswa kubadilishana taarifa na misheni nyingine zinazofanya uangali wa uchaguzi husika, kuwa na uratibu wa kazi zao ni muhimu pia.
- Misheni za ufuatiliaji na uangalizi zinapaswa kuwasiliana na wahusika wote wa mchakato wa uchaguzi na kuitisha mikutano ya kuhabarishana na kujadiliana kiufupi na wadau muhimu au washindani, ikiwa ni pamoja na EMB, vyombo vya habari, vyama vya siasa, mashirika ya kiraia na vikosi vya usalama.
- Wafuatiliaji na waangalizi wanapaswa kutumia kanuni zilizomo katika PEMMO kama msingi wa kutathmini michakato ya uchaguzi katika eneo la SADC.

7.2 Uteuzi na Muundo wa Misheni za Waangalizi wa Kimataifa

Uteuzi na muundo wa misheni ya waangalizi wa uchaguzi ni muhimu ili iweze kuaminika. Vigezo vya uteuzi vinapaswa

kutafuta usawa na kuchanganya uzoefu katika uchaguzi, umri, jinsia na utaifa, hasa waangalizi wa kimataifa. Kutokana na kuendelea kuibuka kwa maeneo/dhima mpya za ufuatiliaji/uangalizi wa uchaguzi, misheni inahitaji kuwa na wataalam wa kiufundi ambao wanaweza kutengeneza zana za kutathmini matumizi ya teknolojia ya uchaguzi, kampeni kupitia mitandao ya kijamii, ufadhili wa kampeni, ushiriki wa makundi yaliyopuuzwa na maeneo mengine. Ikiwa mchakato wa uteuzi hauna uwazi na wala si wa haki, na misheni inakosa uwezo wa kutathmini maeneo fulani ya kiufundi, hii inadhoofisha uwezo wa misheni kufanya tathmini kamili na yenye weledi/utaalam.

Kanuni Zinazopendekezwa

- misheni za uangalizi lazima zihakikishe kuwa washiriki wote wanaweka wazi migogoro yoyote ya kimaslahi kabla ya kushiriki katika misheni.
- misheni za uangalizi lazima ziwe jumuishi na wakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii.
- wahusika katika misheni za uangalizi lazima, kwa pamoja, wawe na ujuzi wa kutosha wa ukanda kwa ujumla na nchi husika inayofanya uchaguzi.
- misheni za uangalizi zinapaswa kufundisha waangalizi husika juu ya matumizi ya PEMMO kama nyenzo ya uangalizi wa uchaguzi.
- misheni za uangalizi zinapaswa kujumuisha wataalam wa uchaguzi kwenye maeneo tofauti tofauti, wataalam wa teknolojia na wapatanishi wa amani, kama mazingira ya nchi husika yatakavyoruhusu.

- misheni za uangalizi wa kimataifa lazima zihakikishe kuwa zina uwiano wa masuala ya kiufundi na kidiplomasia katika misheni zao.
- wakuu wa misheni wanapaswa kuelezwa wajibu wao mapema.

7.3 Mfumo wa Utoaji Taarifa

Mashirika kadhaa ya kimataifa, ya serikali za kikanda na yasiyo ya serikali za kikanda yanahusika katika uangalizi na ufuatiliaji wa uchaguzi katika ukanda wa SADC, ikiwa ni pamoja na ECF-SADC na EISA. Mashirika ya kitaifa yatokanayo na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, FBOs na vyama vya wafanyakazi pia hufuatilia na kuangalia uchaguzi katika nchi zao.

Mijadala ya matokeo ya tathmini imeanza kufuata utaratibu maalum pale ambapo makundi kadhaa yanaangalia mchakato huo wa uchaguzi katika nchi, hata kama yanatumia nyenzo tofauti. Siku ya kupiga kura na kipindi baada tu ya uchaguzi, waangalizi hutoa taarifa (ripoti) kwa umma. Ikiwa taarifa husika zitatolewa kabla ya wakati wake au bila kuzingatia unyeti wa mazingira ya kisiasa yaliyopo, zinaweza kukabiliana na upinzani kutoka kwa wadau wa uchaguzi na Misheni husika kuaibika.

Matokeo ya uchaguzi yanazidi kupingwa mahakamani, kipindi baada tu ya uchaguzi. Bila kutarajia, mashauri yaliyofanikiwa yamesababisha uchaguzi wa rais kurudiwa na kufanyika uchaguzi mdogo. Hii inaonesha umuhimu wa uangalizi makini na utoaji taarifa sahihi baada ya uchaguzi.

Kanuni Zinazopendekezwa

- misheni za uangalizi zinapaswa kuandaa na kusambaza kwa mapana taarifa kwa vyombo vya habari na ripoti kamili na za muda mfupi za tathmini ambazo hazina upendeleo, za kuaminika na zilizoandikwa kwa weledi (kiungwana).
- Misheni za ufuatiliaji na waangalizi zinapaswa kuchukua tahadhari na kufanya maamuzi sahihi katika kuamua ni wakati gani katika msimu wa uchaguzi watoe taarifa kwa vyombo vya habari na ripoti kwa umma, kwa kuzingatia umuhimu wake kwa nchi inayofanya uchaguzi na athari husika kwa mchakato mzima wa uchaguzi.
- Ripoti za misheni za ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi zikitolewa kwa wakati zinaweza kutumiwa kusaidia vyombo vya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi kuzuia au kudhibiti migogoro inayoweza kutokea.

8. Hitimisho

ECF-SADC na EISA wanakiri kwamba utawala wa kidemokrasia ni changamoto kubwa inayokabili eneo la SADC leo, kwa kuwa uchaguzi unachukua nafasi umuhimu sana katika demokrasia. Nyaraka hii inatoa mwongozo kamili wa usimamizi, uangalizi na ufuatiliaji wa uchaguzi katika ukanda huu. Inapendekeza, kiufupi, umuhimu na uharaka wa kuwa na mfumo wa demokrasia unaofanya kazi katika ukanda huu na, hasa, kufanya uchaguzi ambao ni huru, wa haki, halali na wa kuaminika kama moja ya masharti muhimu ya kulea na kuimarisha demokrasia.

Mapendekezo yaliyoorodheshwa hapa chini yamejengwa katika imani thabiti kwamba kupitishwa kwake:

- kutarejesha imani, matumaini na uadilifu muhimu katika usimamizi wa uchaguzi katika ngazi zote;
- kutafanya umma kwa ujumla ujenge dhana thabiti kuwa unamiliki mchakato wa uchaguzi; na
- kutaongeza ushiriki wa watu wa ukanda huu katika chaguzi.

Kwa njia hii, ukanda wa Kusini mwa Afrika utapiga hatua kubwa na za kuigwa katika kufanikisha chaguzi ambazo hazigubikwi migogoro na mabishano (utata). Mapatano haya ni msingi wa amani, utulivu na maendeleo ya kikanda, yote haya yangeongeza thamani katika uimarishaji wa kidemokrasia katika ukanda huu.

Viambatisho

Wanachama wa Kikundi Kazi cha Kurejelea PEMMO

ECF-SADC

Bw. Ulrich Freyer
Kamishna wa zamani wa Tume ya Uchaguzi ya Namibia

Dk Molefe Phirinyane
Kamishna, Tume Huru ya Uchaguzi ya Botswana

Bi. Joyce Laetitia Kazembe
Kamishna, Tume ya Uchaguzi ya Zimbabwe

Bi. Hilda Modisane
Katibu Mtendaji, Sekretarieti ya ECF-SADC

Bw. Bob Musenga
Katibu wa Tume, Tume ya Uchaguzi ya Zambia

Bi. Neena Seewoo
Naibu Afisa Mkuu wa Uchaguzi, Ofisi ya Kamishna wa Uchaguzi wa Mauritius

Bw. Petrus Shaama
Mkurugenzi wa Operesheni, Tume ya Uchaguzi ya Namibia

Bi. Zenia Klazen
Naibu Mkurugenzi wa Usajili na Mipango, Tume ya Uchaguzi ya Namibia

EISA

Bw. Justin Doua Goré
Kiongozi wa EISA katika Mradi wa STEP

Dk. Catherine Musuva
Kiongozi wa zamani wa EISA katika Mpango wa STEP
Mtaalam wa uandishi wa PEMMO

Electoral Commissions Forum of SADC countries (ECF-SADC)

Plot 50669, Unit 1A, Tholo Office Park, Fairgrounds
Private Bag 00284
Gaborone, Botswana
Tel: (+267) 3180012 Fax: (+267) 3180016
Email: info@ecfsadc.org
Website: www.ecfsadc.org

Electoral Institute for Sustainable Democracy in Africa (EISA)

Abidjan, Côte d'Ivoire
Lot numéro 2974, ilot 247 au II
Plateux-7 ème Tranche
Cocody, Abidjan, Côte d'Ivoire

Johannesburg, South Africa
14 Park Road • Richmond 2092
P O Box 740 • Auckland Park 2006, South Africa
Telephone +27 11 381 60 0 Fax +27 11 482 61 63
Email info@eisa.org Web www.eisa.org

Imechapishwa kwa ukarimu na msaada wa kifedha wa watu wa Marekani kupitia kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID)